
**Dk.** Slaa alalamika polisi kukomalia mali zake muhimu

UKURASA 3



**Mganga** jela maisha kwa kumnajisi mwanafunzi

UKURASA 4



**Muhimbili** yamwekea mgonjwa taya jipya

UKURASA 4




**WACHEZAJI YANGA WAAPA KUISHANGAZA AL AHLY KWAO**

UKURASA 24


# Nipashe

Alhamisi Februari 29, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581601

www.ippmedia.com

www.twiter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

The Guardian digital


## KITITA KIPYA BIMA

**Leo wanakuja tena kupunguza gharama za huduma badala ya kuongeza. Wanataka tufe badala ya kusaidia sekta binafsi."- Dk. Makwabe.**





**"Sisi tupo tutaendelea kuzungumza nao kujua malalamiko yao ni yapi na kushauri namna gani ya kufanyia kazi. Yale maeneo ambayo yatahitaji kufanyiwa kazi, yatatekelezwa mara moja." – Bernard Konga**

# NHIF, watoa huduma binafsi bado wavutana

UKURASA 2

# CHADEMA sasa yataka mpango kunusuru hali ngumu maisha

UKURASA 2



Dudley Mbowe akiondoa notisi ya siku 14 iliyowekwa na Dalali wa Mahakama, JJ Auctioneers & Debit Collectors, katika nyumba namba tisa inayodaiwa kuwa mali yake katika Barabara ya Chipata, Mtaa wa Feza, Mikocheni, Dar es Salaam jana, inayotarajiwa kuuzwa kwa mnada kwa amri ya Mahakama Kuu ya Tanzania baada ya kushindwa kulipa deni analodaiwa. **Picha ndogo:** Ni notisi hiyo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mfanyabiashara asusa kusambaza sukari madai maelekezo viongozi

UK. 3

**MICHEZO** **SIMBA WAJIPANGA HUJUMA KWA MKAPA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Makamu Askofu Mkuu wa Kanisa la Kilutheri Afrika Mashariki (KKAM), Askofu Dk. Philemon Langas Mollel (wa pili kushoto) na ujumbe wake, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# NHIF, watoa huduma binafsi bado wavutana

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ukitangaza kuanza kwa matumizi ya kitita kipya kuanzia kesho, Chama cha Wenye Hospitali Binafsi (APHFTA) kimetangaza tena kugomea kuwapa huduma wanachama wa mfuko huo kwa kile kilichoelezwa kupata hasara.

Chama hicho kimesema kuanza kutumika kwa kitita hicho kutazifanya hospitali nyingi binafsi kufa kifo cha asili 'natural death' kwani zitashindwa kujiendesha kutokana na kuongezeka kwa gharama za maisha huku gharama za matibabu zikishushwa.

Hospitali ambazo zinasemekana huenda zisipokee wanachama wa NHIF kuanzia kesho ni pamoja na Kairuki, TMJ, CCBRT, Masana, Regency, Rabinisia, Aga Khan na BOCH.

Taarifa ya chama hicho iliyotiwa saini na Mwenyekiti wake Dk. Egina Makwabe, ilisema pamoja na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuunda kamati teule, hawakushirikishwa na wala hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika kwenye kitita hicho kipya kama walivyolalamika kilipotangazwa awali.

"Kitita kilianza kutumika mwaka 2016 na mpaka mwaka huu hakikufanyiwa mabadiliko yoyote licha ya gharama za maisha kuendelea kupanda.

Leo wanakuja tena kupunguza gharama za huduma badala ya kuongeza wanataka tufe badala ya kusaidia sekta binafsi wanataka kuiua," alisema.

"Kamati iliyoundwa na Waziri wa Afya ilikuwa kama geresha kwa sababu ilikutana na BAKWATA (Baraza Kuu la Waislamu Tanzania) na Chama cha Madaktari Tanzania (MATO lakini sisi hawakutushirikisha. Wamekuja kutupa taarifa mwishoni kabisa baada ya kufanya uamuzi wao na hakuna kilichobadilishwa. Gharama zimeshushwa hospitali binafsi zitajiendeshaje," alihoji mmoja wa viongozi wa APHFTA.

Wakati chama hicho kikitoa msimamo huo, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, akizungumza na jana mkoani Dar es Salaam kuhusu maboresho ya kitita kipya kwa wanufaika wa mfuko huo, alisema utekelezaji wake unatarajia kuanza kesho.

Alipoulizwa msimamo uliotolewa na watoa huduma binafsi kuhusu kitita kipya, Konga alisema: "Sijalipata na kulisoma vizuri lakini ni wenzetu tunakaa mezani majadiliano yanaendelea, majadiliano yapo ni suala endelevu.

"Kuna maeneo ambayo yamekubalika na kuna maeneo hawajakubali tutatekeleza. Kwa yale maeneo ambayo hawayakubali tupo hapa watuletee hata sasa hivi tuyafanyie kazi.

"Ni kweli tusingependa mwanachama yeyote apate shida yoyote na hilo niwahakikishie. Hakuna namna yoyote ambayo mwanachama hatasikilizwa, sisi tupo tutaendelea kuzungumza nao kujua malalamiko yao ni yapi na kushauri namna gani ya kufanyia kazi. Yale maeneo ambayo yatahitaji kufanyiwa kazi, yatayafanyia mara moja."

Alisema tamko hilo watalifuatilia kwa karibu huku akikumbusha kuwa iliundwa kamati maalum ya kitaalamu ambayo ilipokea suala hilo na fursa ya kusikiliza sekta binafsi na serikali.

Konga alifafanua kuwa kitita cha mafao ni orodha ya matibabu ambayo yanatolewa kwa wanufaika wa NHIF na bei zake ambazo hutumika wakati wa malipo kwa madai ya watoa huduma za matibabu.

Alisema maboresho ya mwisho ya kitita kinachotumika sasa yalifanyika Juni, 2016 ikiwa ni takriban miaka minane iliyopita na hivyo kuwapo kwa umuhimu wa kufanya marejeo yake kutokana na sababu mbalimbali.

Konga alisema malengo ya maboresho ya kitita cha mafao yanalenga kuboresha upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama ikiwa ni pamoja na kuongeza huduma ambazo hazikuwapo awali.

"Kufanya maboresho ya huduma na gharama zake kwa kuzingatia maendeleo ya teknolojia na hali halisi ya bei katika soko. Kuwianisha kitita cha mafao na miongozo ya tiba iliyoboreshwa ili kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa wanufaika wa mfuko.

"Kujumuisha maoni na mapendekezo mbalimbali ya wadau.

Kutekeleza ushauri wa taarifa ya mapendekezo ya tathmini ya uhai na uendelevu wa mfuko kwa kipindi kinachoishia Juni 30, 2021, na kuimarisha udhibiti katika mianya ya udanganyifu," alisema.

Konga alisema mfuko ulianza marejeo ya kitita kuanzia mwaka 2018 lakini utekelezaji wake haukufanyika kutokana na uhitaji wa kuhusisha wadau zaidi ili kuwa na uelewa na maoni zaidi kukiboresha.

Alisema maeneo yaliyofanyiwa mapitio na maboresho katika kitita ni, ada za usajili na kupata ushauri wa daktari, huduma za dawa, huduma za vipimo, huduma za upasuaji na gharama za kliniki za kawaida na kibingwa.

"Huduma za usajili na kupata ushauri wa daktari, huwezesha madaktari kufanya kazi katika ngazi zote kutokana na kuwapo kwa usawa wa ada ya kumwona daktari kwa ngazi zote kwa madaktari wa kada zinazoendana.

"Hii itawezesha wanachama kupata huduma za kibingwa katika ngazi mbalimbali za vituo kwa kuzingatia uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali na sekta ya afya.

"Jumla ya dawa 736 zimefanyiwa mapitio kwa kuzingatia bei ya soko na gharama za uendeshaji na wastani wa faida. Hii itaondoa changamoto ya wanachama kukosa baadhi ya dawa na changamoto ya bei," alisema.

Konga alisema maboresho hayo yataongeza upatikanaji wa huduma za dawa katika vituo vya ngazi ya msingi zikiwamo za shinikizo la damu na kisukari.

Pia alisema gharama za vipimo 311 na huduma za upasuaji zimefanyiwa mapitio kwa kuzingatia bei ya soko katika ununuzi wa vifaa na vitendanishi, gharama za uendeshaji na wastani wa faida. Alisema hiyo itaondoa changamoto ya kukosekana kwa huduma za vipimo na upasuaji.

"Kuongeza wigo wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi za upasuaji na vipimo katika hospitali za rufani ngazi ya kanda na taifa. Yataongeza upatikanaji wa matibabu ya saratani, upasuaji wa mifupa, upasuaji wa moyo katika hospitali si za taifa tu bali hata za kanda," alisema.

Alisema katika kuimarisha upatikanaji wa huduma, mfuko umeendelea kudhibiti udanganyifu na kuchukua hatua stahiki kwa wadau watakaodhibitika kujihusisha na vitendo hivyo.

Pia alisema mfuko unaendelea kupokea maoni kutoka kwa wadau hata baada ya kesho na utaendelea kuwajulisha pindi maboresho yoyote yanapotokea ili kuwa na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Mfuko unatoa rai kwa wanachama na mtoa huduma yeyote atakayepata changamoto wakati wa kupata huduma kuwasiliana na mfuko kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa kupiga namna 199 bure au kuwasiliana na Ofisi ya NHIF iliyo karibu," alisema.

# CHADEMA yataka mpango kunusuru hali ngumu maisha

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeomba serikali ipeleke bungeni na Baraza la Mawaziri mpango wa dharura wa kunusuru hali ngumu ya maisha kwa wananchi.

Pia kimesisitiza kuwa maandamano yanayofanyika hayatakoma kwa kuwa ndiyo mbinu pekee ya kuwasilisha hisia za Watanzania kuhusu hali hiyo, hasa uhaba wa bidhaa muhimu kama vile sukari, hivyo kitaendelea kutumia sauti ya umma, kufikisha ujumbe kwa serikali.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, aliyasema hayo Jumatatu wiki hii, katika kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na Kituo cha ITV na kufafanua kuwa mpango huo utatoa suluhu ya kupanda kwa gharama za maisha kwa Watanzania.

"Tuna salamu ya 'no hate na fear' (bila chuki, bila woga). Lakini hii haiondoi ukweli kwamba hasira zetu tunazielekeza wapi! Hasira zetu tunazielekeza kwa kuwaambia watu watumie silaha ya miili yao, kupitia maandamano.

"Kupaza sauti, miili yao inahusika kuonyesha hasira, hisia, tunahimiza watu, sio kuchukulia kila jambo sawa. Sukari haipatikani, ikipatikana bei juu, umeme unakatika, shida ya maji. Mimi nyumbani kwangu kuna shida ya maji miezi hayajatoka hapa Dar es Salaam," alisema Mnyika.

Katibu Mkuu huyo alifafanua kwamba hatua ambazo zinachukuliwa na CHADEMA hivi sasa ikiwamo kuandamana ni kuwaandaa Watanzania katika kile alichokiita kuchagua viongozi sahihi wa kuwaongoza.

"Umma lazima ujiandae kutumia nguvu ya umma kupata viongozi wanaojali maslahi ya watu. Hoja zetu zisikilizwe. Tuna imani utaona namna wanavyojibu, kila mara wanasema maandamano, tunapaza sauti lakini hawasikilizi, hawaoni uzito.

"Maandamano katika majiji yamefanyika nchini, ikiwa ni mwanzo hadi watawala, hususan Rais na Waziri Mkuu, kuzungumza ni lini watapeleka mpango wa dharura huo," alisema.

Kuhusu uchaguzi, Mnyika alisema kwamba, wakati Rais Samia Suluhu Hassan akitarajia kutia saini muswada Sheria ya Uchaguzi kama alivyoahidi, ni vyema marekebisho yafanyike kwenye katiba kama vile suala la wagombea binafsi.

"Vuguvugu la kudai haki, ndiyo kwanza limeanza na watu wanatuunga mkono ambao ndio walengwa wanaokumbana na hali hiyo kila siku. Hali ngumu ni zaidi ya sukari, tunaponyoosha kidole fulani aondoke.

"Ningekuwa mimi Rais kwa hali hii baraza lilikuwa linastahili kuvunjwa. Tujiandae kuwawajibisha zaidi katika uchaguzi, tuwe na sera sahihi," alisema Mnyika.



Licha ya maelekezo ya serikali ya kuwataka wananchi wahame kwenye maeneo hatarishi, bado baadhi yao wanaendelea kuishi kwenye nyumba zilizoharibiwa na mvua, kando ya Mto Mbezi eneo la Kawe Ukwamani, Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wa maisha yao.
**PICHA: SHUKURU MANYAMA**

# Mfanyabiashara asusa kusambaza sukari madai maelekezo ya viongozi

**Na Waandishi Wetu**

MSAMBAZAJI mkuu wa sukari Kanda ya Ziwa, Swami Shreeji, kutoka kampuni ya V.H Shah, amesema amesitisha usambazaji wa bidhaa hiyo kutokana na kile alichokiita kushambuliwa na maelekezo ya viongozi bila kujali anapata kwa gharama gani.

Shah alisema hayo juzi nje ya kikao cha wafanyabiashara wa sukari mkoani Mwanza kilichoitishwa na Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla, baada ya tani 254 kutoka nje zinazosambazwa na Kampuni ya Mohammed Enterprises (MeTL) kuanza kuingizwa mkoani humo.

Alisema amesitisha usambazaji wa bidhaa hiyo kuanzia Februari 15, mwaka huu, kutokana na kuandamwa na maelekezo kutoka kwa viongozi mbalimbali ikiwamo kulalamikiwa kwa nini sukari inayotoka Kagera ipelekwe kwake kwanza ndipo iuzwe kwa wafanyabiashara wa mkoani humo bei zaidi na ile ya Mwanza.

"Kwa sasa sina sukari mimi nimejitoa kwenye sukari maana nashambuliwa. Mfano kauli ya Waziri (wa Kilimo, Hussein Bashe) nadhani mmesikia kuwa sukari inatoka Kagera inakuja Mwanza na Mwanza narudisha Bukoba na kuuza Sh. 150,000 wakati Mwanza ni Sh.140,000. Kutokana na mambo hayo siuzi sukari na pia kiwanda cha Kagera hakinipi tena sukari," alisema.

"Nimejitoa kusambaza sukari tangu Februari 15 labda mpaka na mimi nipewe bei elekezi ya kuchukulia kiwandani maana wanataka niuze mfuko wa kilo 50 kwa Sh.140,000 lakini hawajui nanunua kwa bei gani. Wakiniletea sukari ya Sh.135,000 nitakuwa tayari kuuza wanavyotaka wao," aliongeza.

Akizungumza Februari 22, mwaka huu, katika mkutano uliondaliwa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu jijini Dar es Salaam, Bashe alitaja mtandao wa usambazaji wa wazalishaji hao kuwa sehemu ya uhaba wa sukari nchini.

Bashe alisema wazalishaji hao wana mawakala wachache kiasi cha kuathiri usambazaji wa sukari. Alisema kwa muktadha huo, wakazi wa Kagera hupokea sukari kutoka Mwanza ambayo inasafirishwa kutoka Kagera, hivyo kuongeza gharama zisizo za lazima.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali imewapelekea waraka wenye viwanda ili wabadilishe mifumo ya usambazaji na kuhakikisha kila kiwanda kina kituo cha usambazaji kila mkoa.

Kwa mujibu wa tangazo la serikali Na. 40B lililotolewa Januari 23, mwaka huu, moja ya sukari katika mikoa ya Kanda ya Ziwa inatakiwa kuuzwa kwa bei ya jumla kati Sh. 2,650 na 2,800 huku rejareja ikitakiwa kuuzwa Sh. 2,800 hadi 3,000.

Hali ya serikali kuendelea kukazania bei hiyo elekezi imeonyesha kuwashitua wafanyabiashara walioagiza sukari kutoka nje akiwamo Monica Busumabu aliyesema bei hiyo inawasababishia hasara na kutishia uhai wa biashara zao.

"Nimeagiza tani 31 kutoka kampuni ya MeTL na mfuko wa kilo 50 nimenunua kwa Sh. 140,000 kutoka Dar es Salaam. Hadi kuifikisha huku ukiweka usafirishaji pamoja na mambo mengine, gharama inakuwa kubwa zaidi, hivyo wangeruhusu tuuze hata kwa Sh.155,000 mfuko wa kilo 50,"alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Meneja wa MeLT Mwanza, Roshan Ali, alisema atafikisha wazo la kusambaza sukari hiyo kwa bei ya chini ofisini kwao ili waone namna ya kulipatia ufumbuzi iendane na mahitaji ya bei elekezi.

**KILIO SHINYANGA**

Aidha, wafanyabiashara mkoani Shinyanga, walilalamikia bei elekezi ya serikali wakisema si rafiki kwao, hali inayosababisha kuendelea kuadimika kwa sukari, kutokana na kuogopa kuingia hasara kwa kununua kwa kwa bei kubwa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Seleman Edward, alisema sukari ya Kagera, mfuko wa kilo 50 wanauziwa Sh. 151,000 huku mfuko kwa kilo 25 wakiuza Sh. 75,500 wakati bei elekezi kwa mfuko huo ni Sh. 70,000 sawa na kilo moja kuuziwa Sh.3,200. Kwa bei elekezi, serikali inataka kilo moja iuzwe Sh. 2,800 hadi 3,000.

"Upangaji wa bei elekezi uwe shirikishi kuanzia viwandani, mawakala na wauzaji wa jumla ili mfanyabiashara mdogo akienda kununua sukari ajue bei sahihi ni ipi ili kusaidia kuuza bei iliyoelekezwa na serikali," alisema Albert Msigwa, mfanyabiasha mdogo.

**KAULI ZA MA-RC**

Kutokana na kuingizwa kwa sukari kutoka nje, Makalla aliwaagiza wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na maofisa biashara kufuatilia utekelezaji wa bei elekezi kwa vitendo bila kujali maelezo ya wafanyabiashara ili kuleta unafuu kwa wananchi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mdeme, alisema lengo la serikali ni kuona sukari inashuka bei na ndiyo sababu ikaruhusu uagizaji wa sukari kutoka nje.

**BEI YA SASA**

Licha ya serikali kuruhusu uingizwaji wa sukari kutoka nje huku mkoa wa Mwanza ukiingiza tani 254, bado bei imeendelea kuwa juu. Jana, mkoani Mwanza, wafanyabiashara wa maduka ya jumla waliuza mfuko wa kilo 50 kwa Sh. 180,000 hadi 175,000 na kwa mfuko wa kilo 25 kwa Sh.80, 000 wakitoa sababu kuwa ni gharama za kuchukulia kuwa kubwa zaidi ya bei elekezi.

Ezekiah Stephano, muuzaji wa duka la jumla Mtaa wa Uhuru, alisema bei elekezi ingewafaa na wakaweza kuitumia lakini inawaletea hasara kubwa kutokana na bei wanayochukulia kwa mawakala wao.

Naye Sophia Chacha, muuzaji wa duka la rejareja Mtaa wa Mabatini, alisema kuuza sukari kwa Sh.2,800 mpaka 3,200 kwa kilo moja kama ambavyo serikali imeelekeza ni suala ambalo limekuwa gumu kwake. Alisema bei anayochukulia ya Sh.80,000 hadi 90,000 sawa na wastani wa Sh.3,300 kwa kilo ni tofauti na ile inayoelekezwa.

**•Imeandikwa na Marco Maduhu (SHINYANGA), Zatifa Ramadhan (SAUT), Vitus Audax (MWANZA).**

# Slaa alalamika polisi kukomalia mali zake

**Na Mwandishi Wetu**

IKITIMIA siku ya 199 tangu kuachiwa na Jeshi la Polisi dhidi ya tuhuma za uhaini, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Dk. Willibrod Slaa, amesema hadi sasa hajarejeshewa vifaa vyake vya kielektroniki vilivyochukuliwa na jeshi hilo.

Agosti 13, mwaka jana, Jeshi la Polisi lilimkamata na kufanya upekuzi nyumbani kwake, Mbweni mkoani Dar es Salaam na kuchukua vifaa vyake vya kielektroniki, ambavyo ni kompyuta mpakato (laptop) na iPad , kwa mujibu wa maelezo ya Dk. Slaa.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Dk. Slaa alisema mpaka sasa hajarudishiwa vifaa hivyo ambavyo ni muhimu katika utendaji wake wa kazi.

Dk. Slaa alikamatwa na polisi kwa kile kilichoelezwa kuwa ni uchochezi na baadaye kuunganishwa na Wakili wa Kujitegemea, Boniface Mwabukusi na Mdude Nyagali.

Hata hivyo, kesi yao haikufikishwa mahakamani zaidi ya kutakiwa kuripoti polisi kwa muda waliopangiwa, ingawa hawakufanya hivyo kwa kile walichodai ni usumbufu.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliulizwa kuhusu madai hayo ya Dk. Slaa, alisema vifaa hivyo haviko katika eneo lake la kazi.

"Yeye ameenda kuvidai wapi? Muulize amekwenda kudai wapi? Lini amekwenda kuviulizia? Na ameulizia kwa nani? Na alipewa majibu gani? Na sababu gani alizopewa za kutokurejeshewa?" alihoji Kamanda Muliro.

Mwandishi aliporejea kwa Dk. Slaa kujua undani wa viliko vifaa vyake, alisema aliambiwa kuwa vinashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya.

Alipotafutwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Benjamin Kuzaga, alithibitisha kuvishikilia vifaa hivyo na kumtaka kuvifuata viliko.

"Kama ameambiwa viko Mbeya kwa nini asije? Kwa njia ya kuongea hivi sasa vinarudije? Yeye mwenyewe aje avichukue vitu vyake kama aliviacha huku. Hata tukiongea hapa mimi nafanyaje? Je, nikuhakikishie kwamba, ngoja nivitume? Aje akabidhiwe na kuna taratibu za kukabidhiana," alisisitiza Kamanda Kuzaga.

Dk. Slaa aliwahi kuwa Mbunge wa Karatu na baadaye, Katibu Mkuu CHADEMA, mwaka 2010 aligombea urais na kushika nafasi ya pili akipata kura zaidi ya milioni mbili nyuma ya Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete aliyetangazwa mshindi kwa kupata kura zaidi ya milioni tano.

Alikuwa Katibu Mkuu wa CHADEMA hadi Julai, 2015 alipojiuzulu baada ya chama chake kumpokea Edward Lowassa (sasa marehemu) na kumfanya mgombea wake wa urais, jambo ambalo hakukubaliana nalo.

Novemba, 2017, aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, alimteua Dk. Slaa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Sweden huku alihudumu pia katika nchi zingine za Nordic (Denmark, Finland, Norway) na nchi za Baltic (Estonia, Latvia na Lithuan).

# Mganga jela maisha kunajisi mwanafunzi

**Adela Madyane,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma imemhukumu Kalebo Charles (46), mganga wa kienyeji, kifungo cha maisha na kuchapwa viboko vitano baada ya kumkuta na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa darasa la nne (10) mbele ya mdogo wake.

Charles ambaye ni mkazi wa wilaya ya Buhigwe, alitiwa hatiani baada ya mahakama kuridhika na ushahidi wa watu saba na vielelezo vitatu vilivyotolewa na upande wa Jamhuri kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi, Evelyn Mushi, alisema mtuhumiwa alifanya tukio hilo Septemba 3, 2023 baada ya kumchukua mwathirika na mdogo wake na kuwapeleka katika nyumba ya kulala wageni ya Sebabili iliyoko Manispaa ya Kigoma na kutekeleza tukio hilo.

Hakimu alitoa hukumu hiyo baada ya mtuhumiwa kutenda kosa la ubakaji kinyume cha sheria kifungu cha 130(1)(2)(e) na 131(1) cha kanuni ya adhabu, sura namba 16 ya Sheria za Tanzania kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022. Baada ya hukumu nje ya mahakama, Wakili wa Serikali, Nestory Kuyula, alisema mshtakiwa alifika nyumbani kwao mwathirika kwa lengo la kuwasalimia kwa kuwa ni familia zinazofahamiana na ndipo alipowambia mwathirika na mdogo wake waongozane mahali alipofikia ili akawaone watoto wa mshtakiwa.

Alisema mwathirika huwa anasafiri mara kwa mara kwenda Kigoma Mjini kwa ajili ya kufanya shughuli zake za uganga, hivyo haikuwa ngumu kwake kuambatana naye kwa kuwa ni mtu wanayefahamiana naye ambaye ni rafiki wa familia yake."Walipofika hakukuwa na watoto wa mshtakiwa wala ndugu yeyote ndipo alipombaka mbele ya mdogo wake. Baada ya tendo hilo, mwathirika na mdogo wake walirudi nyumbani na kutoa taarifa kwa bibi yao ambaye wanaishi naye, aliyetoa taarifa kwa mamlaka husika na upelelezi kuanza," alisema.

Alisema hukumu hiyo imetolewa kwa haki na ni fundisho kwa watu wengine wanaofanya ukatili dhidi ya watoto na kuiomba jamii kutoa taarifa kuhusu kila tendo linalofanywa dhidi ya watoto na watu wengine ili haki itendeke.

Kabla ya hukumu, mshtakiwa aliiomba mahakama kumuhurumia na kumpunguzia adhabu kwa kuwa yuko peke yake katika familia na kuna watu anaowalea.



Madaktari Bingwa wa Upasuaji wa Taya na Uso na wataalamu wengine wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), wakimfanyia mgonjwa upasuaji wa kuvuna kipande cha ubavu, jijini Dar es Salaam jana, ili kiwe kiungio cha fuvu kumtengenezea mgonjwa taya jipya na kuwekewa meno bandia. **PICHA: MNH**

# Muhimbili yamwekea mgonjwa taya jipya

**Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), kwa mara ya kwanza imevuna kipande cha ubavu na kukiweka kama kiungio cha fuvu na kumtengenezea mgonjwa taya jipya na hatimaye atawekewa meno bandia.

Upasuaji huo umefanyika jana, kwa saa saba, baada ya mfupa kutoka kwenye ubavu na kutengeneza kiungo na mgonjwa wa kupata taya jipya la kulia, lililoathiriwa na uvimbe.

Bingwa wa Upasuaji wa Uso na Taya MNH, Dk. Arnold Augustino, alisema mgonjwa huyo amefanyiwa upasuaji wa kuondoa taya lote la kulia lililoathiriwa na uvimbe na kumtengenezea taya jipya.

Alisema mfupa ulichukuliwa kutoka kwenye ubavu na mfupa huo umepandikizwa kwenye kiungio cha taya.

"Mifupa mingine imechukuliwa kutoka kwenye nyonga pande zote mbili, ili kuunganishwa na mfupa uliotolewa kwenye ubavu kuwezesha kutengenezwa kwa taya sawa sawa na taya lake la awali.

"Kisha kuunganishwa na kipandikizi cha chuma maalum kutengeneza sehemu ya taya iliyoharibika na ugonjwa," alisema Dk. Augustino.

Bingwa huyo aliongeza kwamba baada ya upasuaji huo, mgonjwa huyo anatarajia kuendelea kula na kutafuna kama kawaida kwa kuwa atawekewa meno bandia kwenye mfupa wa taya aliotengenezewa.

Aliongeza kwamba mgonjwa huyo amefanyiwa upasuaji wa aina tatu tofauti kwa wakati mmoja. Kwanza, alisema alifanyikwa upasuaji kwa kutoa kipande cha mfupa kwenye ubavu, pili kutoa mifupa kwenye nyonga zake zote mbili na tatu kuondoa uvimbe.

Bingwa huyo alisema upasuaji huo ulichukua saa saba kwa kushirikiana shirikisha timu wataalamu wa MNH madaktari bingwa wa taya na uso watano, wataalamu wa usingizi na ganzi wawili, wauguzi wa upasuaji watatu na wataalamu wengine waliokuwapo ni madaktari wanaosomea ubingwa wa kupasua mataya na uso watatu.

Alisema kwa MNH huo ni mwendelezo wa utoaji huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, unaotokana na kujenga uwezo wa wataalamu wazawa chini ya serikali ya sasa ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

## Miili raia wa kigeni yasafirishwa kwao

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imelitaka Shirika la Youth with Mission (YWAM), kutosita kueleza changamoto watakazokutana nazo wanaposhughulikia vibali vya kusafirisha miili ya watu waliopata ajali ya wafanyakazi wao Idara ya Uhamiaji, wanaotarajiwa kupelekwa nchi zao kupumzishwa.

Hayo yalisemwa jana kwenye viwanja vya Shule ya Mchepuo wa Kiingereza New Vision na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emanuela Kaganda, wakati wa ibada ya kuaga miili miwili ya wafanyakazi wa shirika hilo ambao ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo mkoani Arusha John Mukolwe (55), raia wa Kenya na msaidizi wake Vicent Kazungu (36) ambaye ni Mtanzania.

Mukolwe atasafirishwa kesho kwenda Kenya na mazishi yake yatafanyika Machi 9, mwaka huu, na Kazungu alisafirishwa jana kwenda Mwanza kwa mazishi leo wilayani Magu.

Kaganda alisema wilaya hiyo imepoteza viongozi mahiri kwenye idara ya elimu na waliokuwa na ushirikiano mzuri na Halmashauri ya Arusha DC wilayani humo.

Alisema shirika limepata pigo kubwa la kupoteza watumishi wao wa nchi mbalimbali na kuwaomba kushirikisha serikali changamoto watakazokutana nazo wanapojiandaa kusafirisha miili ya wenzao katika nchi zao.

"Hata wale ambao bado wapo mochwari, bado ni viongozi pia wa maeneo yao kwenye nchi zao wa shirika hili, wangetoa michango mikubwa katika jamii zao. Lakini Mungu amekatisha uhai wao hivyo ni pigo kubwa kwa shirika poleni sana.

"Serikali tuko pamoja na ninyi na tutaendelea kusaidia maandalizi ya miili itakayoenda nje kupumzishwa na tumeanza na vibali ambavyo uhamiaji wameanza fanyia kazi na mkipata changamoto mtufahamishe wala msisite, ili kazi ya kuwasafirisha wenzetu nchini kwao ifanyike bila kukwama popote," alisema.

"Hata hivyo nawashukuru wananchi wa eneo la Ngaramtoni wilayani humu ambako ajali hii ilipotokea kabla serikali hatujafika eneo la tukio mlisaidia majeruhi na kuweka ulinzi wa mali za marehemu na majeruhi zisiibwe na hii si Tanzania tu bali kila mahali ajali ikitokea wenye nia mbaya hujitokeza," alisisitiza.

Aidha, alisema Rais Samia Suluhu Hassan na Mkuu wa Mkoa wanaendelea kutoa pole kwa pigo hilo na wapo pamoja hadi pale mtakapopumzisha wapendwa wenu wote kama Rais Samia alivyoelekeza.

Alisema kwa Wilaya ya Arumeru jana imefanya mazishi ya wananchi wake watatu waliopoteza maisha katika ajali hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo Tanzania, Jeremia Kiwinda, alishukuru wadau wa shirika hilo kwa kuchanga Sh.milioni 8.3 kwa ajili ya kusaidia msiba huo.

Pia alishukuru serikali kuwapatia msaada wa jeneza kwa kila marehemu, usafiri na fedha za pole, huku ikisaidia kuhudumia matibabu bure.

# Mpango kupunguza ukatili kingono wazinduliwa

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF), limezindua mpango wa kupunguza kuenea kwa vitendo vya ukatili wa kingono hususan kwa watoto wa kike, kwa kutoa elimu wamiliki na nyumba za kupanga zilizo karibu na maeneo ya shule.

Mkurugenzi Mtendaji wa CDF, Koshuma Mtengeti, alisema hayo jana na kwamba, mpango huo utatekelezwa katika Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma.

"Mradi huu ni wa miaka miwili na utatekelezwa katika kata mbili za Wilaya ya Mpwapwa, Pwaga na Lupeta. Lengo kuu la mradi huu ni kupunguza kuenea kwa vitendo vya ukatili wa kingono kwa watoto hasa wa kike, kuhamasisha jamii kuzuia ukatili.

"CDF litafanya kazi na watoto walioko ndani ya shule, walimu na menejimenti ya shule, viongozi wa serikali, wamiliki wa nyumba za kupanga, wahudumu wa afya, wazazi pamoja na vikundi vya kina baba, ambavyo tunafanya nao kazi," alisema Mtengeti.

Alisema, ili kufikia malengo ya mradi huo, CDF itafanya shughuli mbalimbali zikiwamo, kuwajengea uwezo watoto kwa kuwapa elimu ya afya ya uzazi na namna ya kuzuia ukatili wa kingono.

Kadhalika, aliongeza kwamba, wahudumu wa afya watafikiwa, ili wamudu kutoa huduma bora na rafiki za afya ya uzazi kwa vijana waliopevuka na kuwajengea uwezo wazazi, wamiliki wa nyumba za kupanga zilizo karibu na maeneo ya shule.

"Tutaelimisha madhara ya ukatili kwa watoto, kwa kutumia midahalo, vipeperushi, mikutano ya hadhara na vyombo vya habari. CDF itashirikiana na watumishi mbalimbali wa serikali katika halmashauri ya Mpwapwa," alisema Mtengeti.

Alisema watashirikiana na ofisi ya ustawi wa Jamii, idara ya Maendeleo ya Jamii, idara ya elimu, ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, dawati la polisi la jinsia na watoto, Mahakama ya Wilaya, watendaji kata na Vijiji.

"Lengo kuu la shirika la CDF ni kutekeleza programu na mipango mbalimbali yenye kukuza, kutetea na kuboresha haki na ustawi wa mtoto wa Kitanzania," alisema Mtengeti.




Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir (katikati), akizungumza katika uzinduzi wa huduma za bima ya Takaful zinazofuata misingi ya shariah zinazotolewa na Benki ya CRDB, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Kamishna wa Bima na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware na Ofisa Biashara Mkuu wa benki hiyo, Boma Raballa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Afurahia kupungua uzito kupitia puto

Na Christina Mwakangale

SIKU tano baada ya kuondolewa puto la kupunguza uzito lililomtoa kutoka kilo 151 hadi 92.65, mhusika ametangaza furaha kuondokewa na fedheha.

"Watu walikuwa wakinicheka kutokana na uzito uliokithiri, pia ninataka kuwaasa Watanzania wenzangu wenye matatizo ya uzito mkubwa kuweka puto kunasaidia kupunguza uzito na wasiogope..."

Ni kauli ya Charles Mwakameta, mkazi wa Ngara mkoani Kagera, ambaye ameondolewa puto Jumatatu wiki hii na kupungua uzito wa kilo 58.

Mwakameta aliwekewa puto maalum (intragastric ballon) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila), kwa takribani mwaka mmoja.

Aliwekewa puto hilo Februari 20, mwaka jana, na sasa ana kilo 92.65 akisema safari ya matumaini ilianza baada ya kumwona msanii Peter Msechu kuwekewa puto hospitalini hapo.

Mwakameta alisema amebadilisha mfumo wake wa maisha kwa kuzingatia lishe.

MNH-Mloganzila, ilianzisha huduma ya kupunguza uzito kwa kutumia puto, Novemba 2022, mwaka jana, na hadi sasa walionufaika na huduma hiyo ni 158.

# CRDB imeanzisha huduma za bima zinazozingatia shariah

Na Mwandishi Wetu

IKIWA na uzoefu wa takriban miaka minne sasa, Benki ya CRDB imezindua huduma za bima zinazozingatia misingi ya shariah zijulikanazo kama Takaful kwa ajili ya wateja wanaofuata imani ya Kiislamu na wananchi wengine wanaozingatia misingi ya dini hiyo.

Akizindua huduma hizo, Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kuonyesha njia katika huduma zake kwa kutambua kwamba, wapo baadhi ya wateja ambao hushindwa kupata huduma kutokana na imani zao za kidini.

"Hongereni sana kwa ubunifu huu. Shariah ni sehemu muhimu kwa waumini wa Kiislamu ingawa wapo watu wa imani nyingine wanaozipenda na kuzitekeleza kanuni na misingi ya shariah

"Kwa bima hizi za Takaful, ninaamini mtakuwa mmekata kiu ya wengi, nami ninawaomba Waislamu wenzangu na watu wote wanaoifuata misingi ya shariah kulinda mali na maisha yao kwa bima za Takaful," amesema Sheikh Zubeir," alisema.

Kwa upande wake, Kamshna wa Bima na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, alisema ubunifu unaotatua changamoto zinazowakwamisha Watanzania kutumia huduma za bima unahitajika ili kuikuza sekta hiyo na kuwawezesha wananchi wengi kuwa na uhakika wa mipango na miradi wanayoitekeleza.

"Takaful ni huduma inayowakaribisha watu wenye imani ya Kiislamu ambao hawaridhishwi na huduma za bima ya kawaida ambazo zina riba.

"Takaful sio tu ni huduma za bima bali uwekezaji unaomnufaisha mteja pamoja na kampuni inayotoa huduma hizo. Kwa kutumia mtandao wenu mpana wa matawi, ninaamini CRDB mtazifikisha huduma hizi kila kona ya nchi," alisema Dk. Saqware.

Mwaka 2021 Benki ya CRDB ilianzisha kitengo maalum cha huduma zinazofuata misingi ya Shariah yaani CRDB Al Barakah Banking hali iliyoifanya kuwa benki ya kwanza nchini kufikisha huduma zinazozingatia shariah nchi nzima.

Katika kipindi hicho chote mpaka sasa, CRDB Al Barakah inao wateja zaidi ya 135,000 na kufanya uwezeshaji wa zaidi ya Sh. bilioni 125, sehemu kubwa ikielekezwa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

Ofisa Mkuu wa Biashara wa CRDB, Boma Raballa, alisema siku zote benki inaendelea kuboresha huduma na bidhaa zake na mwaka jana, ilianzisha huduma maalum ya uwezeshaji wa safari za Ibada ya Hijja na Umrah.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mvutano wa NHIF, watoa huduma binafsi utafutiwe ufumbuzi chanya

**MOJA** ya mambo ambayo yanatikisa nchini na kuigusa jamii nzima ya Watanzania ni suala la afya hasa baada ya kuwapo taarifa kwamba Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na wamiliki wa hospitali binafsi, bado wanavutana kutokana na gharama mpya za huduma.

Wamiliki hao kupitia chama chao (APHFTA) wamesema huduma hizo mpya zimeshushwa hali itakayosababisha baadhi yao kushindwa kutoa huduma na hatimaye nyingi kufunga shughuli zao. Sababu kubwa ni kwamba kupunguzwa kwa huduma katika kitita hicho kipya ambacho kinataraji kuanza kutumika kesho, hakuendani na hali halisi ya maisha ambayo yamepanda.

Kwa mujibu wa chama hicho kupitia taarifa yake kwa umma jana na kutiwa saini na mwenyekiti wake, Dk. Egina Makwabe, licha ya suala hilo kuibuliwa na kusababisha mjadala baada ya kutangazwa, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliunda kamati teule kulijadili lakini hawakushirikishwa na wala hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika kwenye kitita hicho kipya kama walivyolalamika kilipotangazwa awali.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alipoulizwa jana katika mkutano wake na vyombo vya habari kuhusu kuanza kwa kitita hicho kipya, alisema alikuwa hajapata taarifa ya hospitali binafsi kugoma kupokea wanachama wa mfuko huo. Hata hivyo, alisema bado kuna nafasi ya kukaa nao na kujadiliana kwa kuwa suala hilo ni endelevu.

Hata hivyo, alisema kuna maeneo watoa huduma hao binafsi ambayo yamekubalika na kuna maeneo hawajakubali na kuwaomba wayawasilishe ili kuyafanyia kazi huku akisisitiza kuwa si nia ya mfuko na wala wasingependa mwanachama yeyote apate shida yoyote.

Pamoja na pande zote mbili kutoa maoni, jambo hilo linaiweka jamii katika hali ya taharuki kwa sababu kama hospitali binafsi zikiwamo Aga khan, Regency, BOCH, Rabinisia, Masana, Kairuki, TMJ na CCBRT zitagoma kupokea wagonjwa ambao ni wanachama wa NHIF, kunaweza kujitokeza tatizo kubwa na hata baadhi ya watu kupata shida.

Huo ndio ukweli kwa sababu hospitali hizo zina huduma za matibabu zikiwamo za kibingwa ambazo baadhi ya hospitali za serikali hazitoa. Pia katika hospitali binafsi hakuna milolongo kama ilivyo kwenye hospitali za umma, hali ambayo huwafanya wagonjwa wengi kukimbilia katika hospitali hizo.

Ushahidi wa wazi juu ya suala hilo ni kufurika kwa wagonjwa katika hospitali hizo binafsi. Kwa mantiki hiyo, kuna uwezekano mkubwa kwa wagonjwa kukosa huduma husika jambo ambalo lawama nyingi zitaelekezwa kwa NHIF. Watu wanafurika zaidi katika hospitali binafsi kwa sababu kuna urahisi wa huduma kulinganisha na zile za serikali ambako kumejaa vikwazo vingi, tuhuma za rushwa zikiwamo.


Mvutano huo baina ya NHIF na hospitali binafsi hauleti afya kwa wananchi ambao wanategemea bima ya afya kujipatia matibabu katika hospitali mbalimbali zikiwamo za binafsi, hivyo ni vyema wahusika wakakaa pamoja na kujadiliana hatimaye kufikia mwafaka kwa manufaa ya Watanzania.

Wahenga wanasema hakuna mshindi katika mgogoro wowote kwa sababu hata yule anayedhani kuwa ameshinda hupata hasara ama ya kiuchumi au ya kijamii kwa kupoteza mambo fulani. Vivyo hivyo, katika hili hakuna mshindi na hapana budi kufahamika kwamba watakaoumia ni wananchi na wadau katika sekta binafsi.

Ni imani kwamba bado kuna nafasi ya NHIF na hospitali binafsi ambao ni mhimili katika utoaji huduma bora za afya kukaa na kujadiliana hatimaye kumaliza tofauti zilizojitokeza kutokana na kitita kipya kwa manufaa ya Watanzania.

Rais Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani, amekuwa akisisitiza kuwa mazungumzo ndiyo njia pekee katika kufikia mwafaka ndiyo maana anasisitiza maridhiano badala ya kutumia nguvu. Kwa hiyo, ni vyema NHIF pia ikakaa na wadau ili kumaliza tofauti zilizoko.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tusikejeli anayofundisha Prof. Janabi kuhusu nafasi ya afya zetu ya kila siku

Na Sabato Kasika

**IDADI** ya wagonjwa wanaofika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya kupata huduma ya kusafisha figo kila siku, ni kati ya 120 hadi 130 na sababu kubwa inaelezwa inatokana na mtindo wa maisha.

Kutokana na hali hiyo, Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Profesa Mohamed Janabi, anahimiza jamii kuchukua tahadhari na kufuata mtindo bora wa maisha kwa kuepuka vitu hatari zaidi kwa afya mwilini.

Prof. Janabi anataja vitu hatari vya kuepukwa kuwa ni sukari na wanga, huku akibainisha kuwa mafuta si hatari kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakidhani, na kwamba mwili hautunzi sukari wala wanga.

Anafafanua kwa kawaida, mwili hubadilisha sukari na wanga kuwa mafuta, hivyo anahimiza watu kupunguza matumizi ya vitu hivyo, na kwamba ugonjwa wa sukari husababishwa na lishe.

Hivyo, anasema, ni lazima jamii ibadilishe mtindo wa maisha na kwamba mtu akibahatika kuzungumza na mgonjwa anayesafishwa figo, ndipo atajua umuhimu wa kujitunza kwa kubadili mtindo wa maisha.

Prof. Janabi amekuwa akitoa mafundisho mara kadhaa kuhusu umuhimu wa kutunza afya, lakini baadhi ya watu wamekuwa wakimkejeli katika mitandao ya kijamii kana kwamba anachofundisha hakina maana.

Nadhani ni vyema kuheshimu taaluma ya mtu na kumsaidia kuhamasisha jamii kuzingatia mtindo mzuri wa maisha, ili kuepuka magonjwa kama hayo ya figo kwa kuepuka vitu vinavyokatazwa.

Kukubali ushauri au mafundisho ya Prof. Janabi ni sawa na kuepuka magonjwa yasiyoambukiza, hivyo, badala ya kukejeli tuchukue hatua zinazoelekezwa na mtaalamu huyo wa afya.

Magonjwa yasiyoambukiza anayataja kuwa ni kisukari, shinikizo la damu, kiharusi na ugonjwa wa figo, ambayo yanaenezwa kwa njia mbalimbali yakitesa baadhi Watanzania.

Itakuwa sahihi iwapo tutaendelea kufuatilia taarifa sahihi za namna ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza, ili kupata taarifa hizo kwa usahihi badala ya kukejeli.

Njia mojawapo ya kufuatilia mafundisho ya Prof. Janabi, ambaye kila mara amekuwa wakitoa rai kwa Watanzania kuzingatia mtindo mzuri wa maisha, ili kuepuka magonjwa mbalimbali yakiwamo yasiyoambukiza.

Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha huduma za afya na inaendelea na juhudi hizo ili kuokoa maisha ya Watanzania ambao wana magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo kutoa matibabu na elimu, hivyo ni wajibu wetu kuzingatia elimu hiyo kwa ajili ya usalama wa afya zetu.

Ikumbukwe, utafiti wa kitaifa wa viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza uliozinduliwa na Wizara ya Afya mwaka jana, ulionyesha kuwa magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) yanachangia takriban asilimia 33 ya vifo vyote nchini.

Pamoja na hayo, takwimu za Shirika la Afya duniani (WHO) kwa mwaka 2020 zikionyesha kuwa magonjwa hayo yalichangia zaidi ya vifo milioni 41 sawa na asilimia 71 ya vifo vyote duniani ukilinganisha na vifo milioni 57 kwa mwaka 2016 duniani.

Hayo ni kwa mujibu wa Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Nassor Mazrui, wakati wa uzinduzi wa utafiti wa kitaifa wa viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza au 'Steps Survey 2023'.

Kwa maana hiyo, suala la kufuatilia mafundisho ya Prof. Janabi na kuyafanyia kazi ni la muhimu, kuliko kukaa kwenye mitandao ya kijamii na kuanza kukejeli kuwa anatisha ili watu wasiendelee kufurahia maisha.

Sasa kwa kuwa serikali inatekeleza mkakati wa kitaifa wa kukabiliana na magonjwa hayo kwa kutoa elimu kwa jamii ya jinsi kujikinga nayo, ninadhani ni wajibu wa kila mmoja kuzingatia elimu hiyo.

HABARI KITAIFA

# Pinda afurahishwa uwekezaji sekta ya afya

**Na Munir Shemweta,** MPIMBWE

MBUNGE wa Kavuu na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanyika kwenye hospitali ya Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi.

Pinda alitoa shukrani hizo juzi alipotembelea na kukagua shughuli zinazofanyika katika hospitali hiyo iliyoko kitongoji cha Tupindo, kata ya Mbede wilayani Mlele. Alisema uwekezaji uliofanyika katika hospitali hiyo hasa vile vifaa vya X-Ray na Utra Sound utachangia kwa kiasi kikubwa kuboreshwa kwa huduma pamoja na kuhudumia wagonjwa kutoka nje ya halmashauri wakiwamo wale wa Sumbawanga vijijini katika maeneo ya Finga, Mtowisa na Muze.

"Nichukue fursa hii kumshukuru sana Rais wetu Mhe, Dkt Samia Suluhu Hassan, amekuwa mama wa kuangalia maisha ya watanzania hususan wananchi wa Mpimbwe kwa kutoa fedha nyingi katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo hili la sekta ya afya, tunataka shida zote ziishie Mpimbwe". Alisema Mhe. Pinda

"Kutokana na uwepo vifaa vya kisasa, tuna uhakika huduma za afya zinaendelea kuimarika na niwatake muimarishe usafi katika maeneo yanayozunguka hospitali" aliongeza Mbunge huyo wa jimbo la Kavuu.

Mganga Mfawidhi wa hospitali ya Halmashauri ya Mpimbwe (Tupindo) Dkt Rio Ernest amesema, hospitali hiyo kwa sasa inavyo vitengo mbalimbali vyenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa na kuvitaja kuwa ni kitengo cha Afya ya kinywa, Macho, Mionzi, Wazazi, Maabara pamoja na Wagonjwa wa nje na ndani. "Hospitali hii pia inacho kitengo cha dharura chenye vifaa mahsusi kwa wagonjwa wa dharura huduma ambazo kwa sasa zimeunganishwa na wagonjwa wa dharura suala linapunguza ufanisi katika idara hiyo". Alisema Dkt Rio

Hata hivyo, ameeleza kuwa, pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanyika zipo changamoto kadhaa kama vile uchache wa watumishi jambo alilolieleza kuwa linapelekea baadhi ya vitengo kutofanya kazi kwa saa 24 na kutolea mfano wa vitengo vya Famasia, Mionzi na Maabara.

Ametaja changamoto nyingine kuwa ni barabara za ndani ya hospitali sambamba na ukosefu mitaro ya kutoa maji ndani ya eneo la hospitali. Pia ukosefu wa uzio unaosababisha usalama kwa wagonjwa, watoa huduma na mali za hospitali.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mpimbwe, Shamim Mwariko, alimweleza Pinda kuwa uwelezaji uliofanyika katika hospitali hiyo umesababisha kuongezeka kwa mapato ya hospitali.

"Kuongezeka vifaa kumesababisha kuongezeka wateja, hivyo kuchangia ongezeko la mapato ya hospitali. Julai, mwaka jana, mapato yalikuwa Sh. milioni mbili na sasa tunakusanya Sh. milioni saba," alisema. Hospitali ya Halmashauri ya Mpimbwe ilianza kutoa huduma mwaka 2020 na sasa inaendelea kukua kwa kasi kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (kushoto), akizungumza na wajumbe ya kamati ya ulinzi na usalama iliyoambatana na viongozi wa kata, baada ya kufanya ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa zahanati inayojengwa katika Kata ya Kiwanja cha Ndege, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Nchi Afrika Mashariki zakubaliana usimamizi madhubuti miradi umeme

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mawaziri wanaohusika na mfumo wa pamoja wa umeme kwa nchi za Mashariki mwa Afrika (EAPP) limekubaliana kwa pamoja kuwa na usimamizi madhubuti wa miradi mbalimbali ya umeme katika nchi wanachama, ili kukamilika kwa wakati na kuwapatia wananchi nishati ya kutosha.

Kukamilika kwa miradi kutoka vyanzo mbalimbali vya umeme, kutawezesha nchi hizo kusaidiana pale nchi mojawapo inapokuwa na upungufu wa nishati hiyo huku msisitizo ukiwekwa kwenye miradi ya usafirishaji wa umeme. Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayo juzi katika Mkutano wa 18 wa EAPP uliofanyika kwa siku mbili Nairobi, Kenya.

"Baraza hili ni muhimu katika kuhakikisha nchi za Afrika zinaungana kwa ajili ya kuendeleza rasilimali za umeme zilizopo pamoja na kupata umeme wa uhakika kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. katika mkutano huu kila nchi imeonyesha utayari kufanya biashara ya umeme pale kunapokuwa na umeme wa ziada," alisema.

Dk. Biteko alisema kuna idadi kubwa ya watu katika nchi wanachama wa EAPP, hivyo inahitajika nishati zaidi kwa ajili ya maendeleo ya watu na viwanda na ndio maana kila nchi imejikita katika kuendeleza vyanzo mbalimbali vya umeme ajili ya kujipatia nishati ya uhakika. Alisema Tanzania itakuwa sehemu ya soko la umeme pale nchi jirani zitakapohitaji nishati hiyo baada ya kuwashwa kwa mashine zote tisa katika Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere litazalisha megawati 2,115 ambazo zinatoa uhakika wa kutosheleza mahitaji ya ndani.

"Tanzania kuna njia mbalimbali za usafirishaji umeme. Mfano Tanzania na Uganda, Tanzania na Burundi pamoja na Tanzania na Rwanda na sasa kuna laini ya umeme kutoka Tanzania hadi

Kenya ambayo imekamilika na iko kwenye majaribio itakayotuwezesha kufanya biashara kati ya nchi hizi mbili pale kila nchi ikiwa na umeme wa kutosha," alisema.

Aliongeza kuwa kuna upembuzi yakinifu unafanyika chini ya Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kujenga mradi mkubwa wa usafirishaji umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda kutoka Shinyanga. Alisema mradi huo utasafirisha umeme mwingi zaidi kwa baadhi ya mikoa kama vile Kagera na pia kuwezesha nchi hizo kufanya biashara ya umeme.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko amesema kuwa, Sekta ya Nishati ni injini katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii, hivyo suala la kupeleka nishati ya kutosha, salama na ya gharama nafuu kwa wananchi si suala la hiari bali ni wajibu kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na kijamii.

Ameeleza kuwa, ukuaji wa Sekta ya Nishati kwa nchi za Mashariki mwa Afrika ni asilimia 6 kwa mwaka, hivyo bado kuna kazi kubwa ili kuhakikisha wananchi katika nchi hizo wanapata nishati ya uhakika na kwa gharama nafuu.

Amesema chini ya mfumo wa pamoja wa umeme EAPP kuna miradi mbalimbali iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa kuimarisha upatikanaji wa nishati katika nchi wanachama akitolea mfano mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umeme wa Kenya-Uganda, Kenya-Ethiopia, Kenya-Tanzania, Tanzania-Rwanda, Tanzania-Uganda, Tanzania-Burundi na DRC-Burundi. Alisisitiza kuwa nchi wanachama zinapaswa kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati ili kupunguza changamoto za umeme kwa kuwa nishati hiyo inaweza kusafirishwa kutoka eneo moja kwenda lingine na

kuwezesha upatikanaji wa huduma hiyo kwa uhakika.

Awali, Mwenyekiti wa kikao hicho na Waziri wa Nishati na Petroli wa Kenya, Davis Chirchir, alisema lengo la nchi kuwa na mfumo huo ni nchi wanachama 13 kufanya mauziano ya umeme pale kunapokuwa na ziada na kwamba ili suala hilo liwezekane lazima kuwapo na miundombinu inayounganisha nchi hizo.

Alisema majadiliano ya viongozi hao yamelenga katika kuimarisha muundo wa umoja huo pamoja na ushirikiano na hii ikijumuisha namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za umeme pale zinapojitokeza.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, Kenya tayari inafaidika na mfumo huo wa umeme baada ya kupokea magawati 200 kutoka Ethiopia, hivyo kuongeza kiasi cha umeme katika nchi hiyo.

Aliongeza kuwa ameongeza kuwa, takriban watu milioni 600 bado hawajapata nishati umeme barani Afrika kati ya watu takriban bilioni 1.5 na hiyo inaonyesha nguvu zaidi inavyohitajika ili kuwa na nishati ya kutosha kukidhi mahitaji.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



# Makazi ya Nyerere kuwa kituo cha utalii

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imedhamiria kufanya makazi ya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, yaliyoko kijiji cha Mwitongo, wilayani Butiama mkoani Mara kuwa kituo cha utalii.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wakati akizungumza na wakazi wa Kitongoji cha Muhumba, wilayani Butiama, akiwa njiani Kwenda Mugumu, Serengeti ambako anaendelea na ziara yake ya kikazi mkoani Mara.

Waziri Mkuu Majaliwa alimwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo, Moses Kaegele, atembelee eneo, akague na kuangalia kasoro zilizoko ili serikali izifanyie kazi.

Pia aliiagiza Wizara ya Ujenzi ishughulikie barabara ya kutoka Serengeti hadi Butiama ili ikamilike na kuwawezesha watalii wanaotaka kufika kwenye makumbusho hayo kwa njia ya barabara.

Waziri Mkuu alipitia Mwitongo na kuwasalimia wanafamilia wa Baba wa Taifa na kuweka shada la maua kwenye kaburi lake.

Mapema, alipowasili wilayani humo, Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama ambayo utekelezaji wake umefikia asilimia 60.

Akizungumza baada ya kuweka jiwe hilo, Waziri Mkuu alimtaka mkandarasi wa mradi huo ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ahakikishe anaukamilisha mradi huo kwa wakati. Hadi sasa, mkandarasi ameshalipwa Sh. milioni 843.4 ikiwa ni malipo ya awali na hati za malipo ya pili na tatu.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alisema Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inaendelea na kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji ambapo kazi kubwa imefanyika na sasa nguvu kubwa inaelekezwa kwenye kufikisha umeme kwenye vitongoji.

Akizungumza na wakazi wa Issenyi, wilayani Serengeti, akiwa njiani kuelekea Mugumu, Mheshimiwa Majaliwa alitoa rai kwa Watanzania waachane na matumizi ya kuni na mkaa na badala yake waanze kutumia gesi.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, akiongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano wa 13 wa Mawaziri wa Biashara unaoendelea, Abu Dhabi, Falme za Kiarabu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yatoa msimamo kuhusu WTO

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA imesema inaunga mkono mfumo wa biashara unaotegemea Sheria ambazo zinatoa ulinzi na fursa kwa nchi wanachama wote hasa nchi zinazoendelea katika kuhakikisha maendeleo endelevu duniani yanapatikana.

Vilevile, Tanzania ambayo ni miongoni mwa nchi waanzilishi wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) imesema inaunga mkono maboresho ya shirika hilo yanayohakikisha maslahi ya usawa ya nchi wanachama na hasa zile zinazoendelea.

Msimamo huo ulitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah wakati akitoa msimamo wa Tanzania katika Mkutano wa 13 wa Mawaziri wa Biashara, unaoendelea katika ukumbi wa Mikutano wa ADNEC, Abudhabi katika Falme za Kiarabu.

Alisema nia ni kufikia lengo pana la ushirikishwaji na kukuza maendeleo endelevu kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Marrakesh wa kuanzisha WTO.

Aidha, alisema Tanzania inaendelea kusisitiza kuwa matokeo ya mafanikio ya maboresho hayo yanapaswa kuwa sawa na kuzingatia mahitaji tofauti ya wanachama kulingana na tofauti zao za uchumi na maendeleo.

Alisema kuna haja pia ya kulenga kurekebisha baadhi ya sheria za biashara ambazo kwa namna fulani zimesababisha kufa kwa viwanda katika baadhi ya nchi wanachama.

Kuhusu Mkataba wa Ruzuku kwa wavuvi, Dk. Abdallah alisema Tanzania itahakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinavunwa kwa njia endelevu na rafiki kwa kuwa kwa nchi nyingi zinazoendelea, sekta ya uvuvi ndiyo nguzo ya ajira kwa jamii zinazozunguka maeneo ya maji.

Alisema hiyo imesaidia kuwa chanzo cha mapato na chakula kwa maisha ya vijijini na mijini na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

Alisema ni muhimu kuhakikisha mkataba huo unajumuisha matibabu maalum na tofauti yanayofaa ikiwa ni pamoja na misaada ya kiufundi na kujenga uwezo kwa nchi hizo zinazoendelea.

"Uvuvi ni shughuli muhimu ya kiuchumi kwa Tanzania na ina ufukwe wenye urefu wa kilomita 1,424 na eneo la kiuchumi la pekee la kilomita za mraba 223,000 ambapo sekta ya uvuvi inawaajiri wavuvi wapatao 200,000 wa moja kwa moja na jumla ya samaki wanaovuliwa ni tani takriban 415,000 kwa mwaka," alisema Dk. Abdallah.

Aidha, katika hatua nyingine, Dk. Abdallah alisisitiza hatua za kuhakikisha usalama wa chakula, zinakuwa jumuishi katika kushughulikia mahitaji katika mnyororo wa thamani.

Alitaja hatua hizo kuwa ni pamoja na teknolojia mpya zinazohusiana na uzalishaji wa vyakula vya msingi, usindikaji, uhifadhi na uuzaji wa bidhaa za kilimo ambazo kwa upande wake zitaathiri vyema uzalishaji, ushindani na maisha ya wakulima na jamii za vijijini katika nchi zinazoendelea.

## Wasiojulikana waua dereva wa bodaboda

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawasaka watu wasiojulikana waliomuua kwa kumkata mapanga mwendesha bodaboda, Cassian Laiti (36), kisha kuiba pikipiki aliyokuwa anaendesha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi (ACP) Shadrack Masija, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea Februari 24, majira ya saa 5:30 usiku katika mtaa wa Familia Takatifu, kata ya Kizwite, Manispaa ya Sumbawanga.

Alisema kabla ya mauaji hayo watuhumiwa hao walikodi pikipiki ya Laiti na kupanda mshikaki wakimtaka awapeleke nje ya mji kwa kuwa walimshawishi kwa kumlipa fedha nyingi naye akakubali asijue kama ulikuwa mtego.

"Walipokuwa wakielekea huko, walifika katika mtaa wa Familia Takatifu ndipo walipomfanyia tukio hilo la kumkata mapanga kisha kuuacha mwili wake barabarani na kuondoka na pikipiki aina ya Kinglion yenye namba za usajili MC 173 DEL na kutokomea nayo kusikojulikana," alisema.

Alisema asubuhi, wakazi wa mtaa huo waliuona mwili wa marehemu na kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa mtaa naye akawaita polisi ambao walifika eneo la tukio na kuuchukua mwili kisha kuwakabidhi ndugu zake kwa ajili ya maziko.

Kamanda Masija alitoa wito kwa waendesha bodaboda kuchukua tahadhari pindi wanapofanya kazi hiyo nyakati za usiku pia wasiwe wanabeba abiria mshkaki kwa kuwa ni hatari kwa usalama wao na abiria.

Alisema polisi wanaendelea na upelelezi wa tukio hilo ili kuwabaini watuhumiwa wa mauaji hayo na watakapokamatwa watafikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.



## HABARI KASKAZINI

# Serikali kufumua menejimenti vyuo vikuu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolph Mkenda, amesema hajawahi kuona faida ya kuwa na Makamu Mkuu wa Chuo Utafiti (DVC Research) katika vyuo vikuu kwa kuwa sehemu nyingine wamekuwa kikwazo cha watafiti kwa sababu wanafikiri wao ni mamlaka ya mapato.

Kutokana na changamoto hiyo, amesema serikali itazungumza na vyuo vikuu nchini, kuangalia uwezekano wa kufuta cheo hicho na kukirudisha kuwa chini ya Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma.

"Wana frustrate resechers (kuvuruga watafiti), nadhani tutakuja kuongea uwezekano wa kufuta kile cheo kirudi kwa DVC Academic (Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma). Na kwa kweli ukija ukiuliza wana vyuo au wale wahadhiri, watakuambia sisi hatuoni faida hiyo, sana sana tu ni kuongeza resources (rasilimali)." Alikuwa akizungumza jana na Wahadhiri katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kabla ya kukagua miradi mikubwa miwili ya ujenzi wa jengo la maktaba lenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2,500 wa wakati mmoja na ujenzi wa jengo la ghorofa lenye kumbi za mihadhara na ofisi lenye uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi 1,800.

"Nazungumzia vyuo vikuu vyote kwamba tuna haja sana ya ku-strimeline shughuli za central administration (kupunguza madaraka). Kuna ka-tendence (katabia) kamekuwa kakitokea. Nitatoa mfano tu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa sababu mimi nimeajiriwa kule na nimefanya kazi muda mrefu sana.

"Tulikuwa wakati ule tuna vitivo na central administration (utawala), halafu ikaamuliwa kwamba madaraka yashuke chini kidogo kwenye vitivo ku-decentralize (kushusha madaraka). Sasa maamuzi hayo yalifanyika na vitivo hivyo vikaitwa college (ndaki), na nyingine zikaitwa shule kuu.

...Nakumbuka siku tunazindua Ndaki ya Arts of Social Sciences, tulimuita Mheshimiwa Museveni (Yoweri-Rais wa Uganda) kwa sababu alisoma pale na alikuja kuzindua. Tulisema kwa nini tunafanya hivyo, ni ili mambo mengi tuyashushe huko chini. Kwa hiyo kazi ilifanyika ikakamilika halafu mambo mengi yakachukuliwa chini yakapandishwa juu."

Akifafanua zaidi, Waziri Mkenda, alisema kuna katabia kakutaka kuanzisha kurugenzi, halafu watu wanasahau tunatakiwa kuimarisha zile sehemu ambazo ni za ufundishaji na utafiti.

"Na kwa kweli kwa maoni yangu mimi, hata hii inaitwa DVC Research ni ya kuvunja. Na hili tutajaribu kulizungumza ili kuondosha. Kwa sababu ukiwa na Vice Chancellor, ukiwa na Deputy Vice Chancellor Academic, Academic sio teaching tu ni pamoja na research.

...Halafu unakuwa na vice chancellor Admistration halafu Vice Chancellor Reaseach, halafu kwenye Vice Chancellor Research kuna Mkurugenzi wa Research, halafu Vice Chancellor Academic kuna Mkurugenzi wa Post Graduate, kuna Mkurugenzi wa Undergraduate.

Zamani pale kwa VC Academic, kulikuwa kuna Mkurugenzi wa Reseacher, Mkurugenzi wa Post Graduate na Under Graduate na kazi zilikuwa zinakwenda. Sijawahi kuona faida ya kuwa na DVC Research.

Aliongeza: "Tena sehemu nyingine, DVC Research imekuwa ni kikwazo cha watafiti vyuo vikuu, kwa sababu kazi yao wanafikiria wao ndio TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), kazi yao ni kukusanya revenue (mapato) kutoka kwa researchers (watafiti).

"Wana frustrate reseacher's, nadhani tutakuja kuongea uwezekano wa kufuta kile cheo kirudi kwa DVC Academic."

Makamu Mkuu wa MoCU, Profesa Alfred Sife, alimweleza kuwa chuo hicho kinakabiliwa na upungufu wa wahadhiri na watumishi waendeshaji ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Prof. Sife, alisema MoCU inakabiliwa pia na upungufu wa kumbi za mihadhara, vyumba vya semina, maabara za kompyuta na ufinyu wa nafasi katika maktaba za chuo ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi.

Nyingine ni uchakavu wa majengo na miundombinu ya kufundishia na kujisomea, uhaba wa mabweni ya wanafunzi na miundombinu isiyokidhi mahitaji ya watu wenye mahitaji maalumu.




Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Taifa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (MNEC), Rehema Omari (mwenye kipaza sauti), akizungumza baada ya kufungua tawi la wakereketwa la UVCCM la Mlimani Park, katika Mtaa wa Mdote, Kata ya Majengo, Wilaya ya Muheza mkoani Tanga jana. Wengine ni Diwani wa kata hiyo, Mukadam Sabuni (kushoto), Mwenyekiti wa UVCCM wilaya, Hadija Mshakangoto (wa pili kushoto) na Katibu Tawala wilaya hiyo, Mohamed Mfaki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanavijiji Amani wapata neema

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

WAKAZI wa vijiji vinavyozunguka Hifadhi za Mazingira Asilia ikiwamo ya Amani mkoani Tanga wameanza kubadili maisha yao kwa kuongeza kipato kutokana na uwekezaji katika ufugaji wa nyuki, samaki na utengenezaji majiko banifu.

Miradi hiyo ni ile inayofadhiliwa na Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) kwa gharama ya Sh. milioni 600 kwa mwaka.

Akizungumzia uwekezaji huo, Mkazi wa Kijiji cha Shebomeza kilichoko Kata ya Amani Wilaya ya Muheza, Zabibu Rajabu, alisema wameanza kuvuna mazao ya mboga na viungo kutokana na kuwekeza katika mradi wa hifadhi ya ardhi na maji shambani.

Zabibu, alisema kupitia wataalamu wa kilimo, wakazi wa kijiji hicho, wamefundishwa kilimo cha makinga maji na kuzuia mmomonyoko wa udongo.

"Kwa sasa tunaweza kupanda mazao mbalimbali ikiwamo mahindi, nanasi, miwa na parachichi. Nilikuwa sivuni mahindi, ila sasa navuna kwani mvua inapokuja maporomoko yanakuwa hayapo tena. Maji yanapotoka juu yanaishia kwenye kingamaji, yanapita kwenye mfereji, hayaendi kwa kasi," alisema.

Katibu Tawala Msaidizi, Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga, anayeshughulikia uzalishaji, Emigidius Kasunzu, alisema wakazi wa vijiji vinavyozunguka maeneo hayo, wamepatiwa miradi hiyo rafiki na kujiongezea kipato na kuendelea kuhifadhi mazingira.

"Mfuko umesaidia kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabia nchi, uhifadhi na miradi mingi ambayo inawasaidia wananchi kupata kipato. Kuanzia mwaka 206 mkoa tunapata kila mwaka shilingi milioni 600 ambazo zinaenda moja kwa moja kwa wananchi," alisema.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Muheza na Mratibu wa Mradi huo, Sylvester Mziray, alisema ulianza mwaka 2016 na hadi sasa wakulima 120 wavijiji vitatu, wamenufaika na elimu ya kilimo hicho.

# Jela miaka 60 kwa kubaka wasichana kwa zamu

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani hapa imemhukumu kifungo cha miaka 60, Mkazi wa Kijiji cha Mandi, Jeremia Lorri (45) baada ya kupatikana na hatia ya kuwabaka wasichana wawili kwa zamu.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, alisema mahakama yake imemtia hatiani katika makosa mawili ya ubakaji. Hakimu Kimario alisema kuwa siku ya tukio hilo, mshtakiwa huyo aliamua kujifungia dukani kwa mmoja wa wasichana hao (majina yanahifadhiwa) na kuanza kuwabaka kwa zamu.

Alisema mshtakiwa huyo anadaiwa kufanya unyama huo Desemba 10, mwaka jana katika kijiji hicho kilichoko katika wilaya hiyo usiku kucha na kuondoka dukani humo saa 11:00 alfajiri.

Kwa mujibu wa Hakimu Kimario, mshtakiwa huyo, ametiwa hatiani baada ya mahakama hiyo kiridhika pasipo shaka kuwa alitenda kosa hilo. Upande wa mashtaka katika kesi hiyo, uliwatumia mashahidi sita na vielelezo viwili, huku mshtakiwa huyo akijitetea mwenyewe. Alisema ushahidi wa mabinti watatu wakiwamo waliofanyiwa unyama huyo, uliendana na maelezo ya mashahidi sita na hivyo, mahakama hiyo kumtia hatiani mshtakiwa huyo. Hakimu Kimario, alisema mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 130 (1), (2) (e) na kifungu cha 131 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022.

Awali Wakili wa Serikali, Raphael Rwezahula, akisaidiwa na Wakili Mwanaidi Chuma, alisema kuwa mshtakiwa hana kumbukumbu za uhalifu huko nyuma dhidi ya mshtakiwa huyo na kuiomba mahakama kumpa adhabu kali kwa kuwa alibaka msichana wa miaka 14 na wa miaka 15, kitendo ambacho kinawaathiri kisaikolojia.





# Wafugaji walilia majosho kila kijiji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAFUGAJI wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani hapa wameiomba serikali kuwajengea majosho ya kuoshea mifugo kila kijiji ili kuwaondolea gharama na adha ya kufuata huduma hiyo mbali na maeneo yao na kupulizia dawa kiholela.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya CCM ya wilaya hiyo ya kukagua miradi ya maendeleo ukiwemo ujenzi wa josho la Solwa.

Mfugaji Sangija Musa, alisema wamekuwa wakishindwa kwenda kuogesha mifugo yao kwenye majosho hayo yenye dawa kutokana na kujengwa mbali na makazi yao hivyo kuamua kunyunyizia dawa ambayo si salama.

Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Edward Ngelela, alisema kwa mujibu wa wataalamu wa mifugo, kuogesha mifugo katika majosho yenye dawa kunanusuru mifugo dhidi ya magonjwa.

Ngelela, alisema mifugo inapoingizwa kwenye josho na kunasaidia kufikiwa na dawa kila eneo la mwili na kuua wadudu wawasumbua tofauti na kunyunyizia dawa.

Aliwaagiza maofisa mifugo wa halmashauri hiyo kutoa elimu kwa wafugaji ya umuhimu wa kuongesha mifugo kwenye majosho ili iwe salama kwa kukingwa na magonjwa.

Ofisa Mifugo Kata ya Solwa, Lukali Marick akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa josho hilo kwa kamati hiyo, alisema ulikamika Desemba mwaka jana kwa gharama ya Sh. milioni 23.

Marick, alisema josho hilo litahudumia vijiji vya Solwa, Mwadutu, Mwasekagi na Mwisemi na kwamba halmashauri hiyo haina mpango wa kujenga majosho hayo kila kijiji mpaka bajeti itakapopangwa.

# Wachimbaji wanaodaiwa kuvamia mgodi waitega serikali Shinyanga

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa Kijiji cha Maghung'hwa Kata ya Mwakata Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga wameitega serikali wakisema watahama eneo la mgodi wanalodaiwa kuvamia baada ya kutekeleza ahadi ya kuwatafutia maeneo mengine katika kipindi cha miezi mitatu.

Wachimbaji hao wadogo wanadaiwa kuvamia maeneo ya mgodi huo unaomilikiwa na mwekezaji wa kampuni ya Ganuck na kuanzisha shughuli za uchimbaji kwa maduara 21.

Inadaiwa kuwabaada ya kugundulika wakifanya uchimbaji huo kinyume cha sharia, maduara hayo yalifungwa Januari 11 mwaka huu.

Akizungumza juzi na wachimbaji hao katika mkutano wa hadhara, Naibu Waziri wa Madini Dk. Steven Kiruswa, alisema serikali imeamua kuingilia suala hilo ili kutatua mgogoro uliopo baina yao na mwekezaji huyo anayemiliki leseni ya eneo hilo.

Dk. Kiruswa, alisema waliingia makubaliano na mwekezaji huyo kuwa wachimbaji hao wasaini mkataba wa kuendelea na shughuli zao kwa muda wa miezi mitatu wakati serikali ikiwatafutia eneo lingine.

Alisema kuwa makubaliano hayo yatasainiwa na mmiliki wa mgodi huo, Ofisi ya Madini Mkoa wa Kahama na wachimbaji hao kwa kila kikundi cha uchimbaji.

Naibu Waziri huyo alionya kuwa wachimbaji watakaokiuka mkataba huo, baada ya kuisha wataondolewa kwa nguvu.

Aliwataka wachimbaji hao kuunda vikundi vya watu kuanzia 10 na kuendelea kwa ajili ya kupewa maeneo mengine ya uchimbaji na kuomba leseni ya umiliki mtandaoni.

Alimtaka Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa huo, Joseph Kumburu kuwapatia wachimbaji hao maeneo yaliyofanyiwa utafiti na yenye uzalishaji.

Mbunge wa Msalala, Iddi Kassim, aliwataka wachimbaji hao kutumia muda huo waliopewa kuzalisha dhahabu kwa wingi ili kupata fedha za kurejesha mkopo na kuwekeza kwenye uchimbaji wa madini wakati serikali ikiendelea kuwatafutia eneo lingine la uchimbaji lisililokuwa na mgogoro.

Awali akitoa taarifa yake, Meneja wa Canuck, Devid Degratius alisema kuwa kati wananchi 75 waliotakiwa kulipwa fidia na kuondoka kwenye eneo hilo, 71 walikabidhiwa fedha, lakini wanne walikataa.

Degratius, alisema wananchi hao waliokataa ndio waliowakabidhi wachimbaji hao kwenye maeneo yao kuanzisha uchimbaji.

Alisema wanataka wachimbaji hao waondoke kwenye eneo hilo kwa sababu wanaingiliana kwenye uzalishaji chini kwa chini na kushindwa kuvunja miamba kwa baruti kwa kuhofia maisha yao.

Akizungumza kwa niaba ya wachimbaji hao, Juma Kanji aliahidi kuwa watatii mkataba huo na kuwa muda kuondoka ukifika, wataondoka endapo serikali itawapatia maeneo hayo ya kudumu.




Kamanda wa Polisi mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi akionyesha mifuko nane ya ya sukari kwa waandishi wa habari, mkoani humo juzi, waliyoikamata kutoka kwa mfanyabiashara mmoja, wilayani Kahama akimuuzia mwananchi kwa bei ya juu na kukiuka bei elekezi ya Serikali. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Viumbe hai majini hatarini kutoweka

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

VIUMBE hai wakiwemo samaki wapo hatarini kutoweka kutokana na shughuli za kilimo zinazoendelea kuharibu vyanzo vya maji mkoani Kagera.

Hayo yamebainishwa na Meneja wa Bonde la Ziwa Victoria Kanda ya Kagera, Revodius Bishanda wakati akizungumza na Nipashe juu ya athari za kimazingira zinazosababishwa na shughuli za kibinadamu zinazoendelea kwenye vyanzo hivyo.

Bishanda alikitaja kilimo kuwa kinara katika uharibifu wa ikolojia ya viumbe hai wa majini na kusababisha kupotea kwa baadhi ya mazalia yake.

"Hii inatokana na kutifua udogo kwenye eneo la vyanzo hali inayoweza kusababisha eneo husika kujaa udongo na kupoteza asili yake ya maji hali inayosababisha maji kusambaa mahali ambako haikustahili na viumbe hai wanaotegemea maji hayo kukosa uhai," alisema Bishanda.

Alisema mkulima anawaza kupata faida na sio athari ya kusababisha chanzo cha maji kukauka na kuathiri viumbe wengine endapo eneo likikimbwa na ukame.

"Kina cha maji kikipungua kwa kusababishwa na binadamu aliyeona uzalishaji ni muhimu kuliko uhai wa wengine matokeo ya haraka utaanza kuona mabadliko ya tabia ya nchi kama ukame," alisema.

Aliwataka wakulima kuacha kufanya shughuli za kilimo kando ya chanzo chochote cha maji kwani ni kinyume cha sheria na kuonya kuwa atakayebainika sheria kali zitachukuliwa dhidi yake.

Mkazi wa Kata Bakoba Manispaa ya Bukoba, Sauli Thomas, alisema amekuwa akifanya shughuli za kilimo kando ya mto kwa miaka saba kwa ajili ya kujipatia kipato bila kufahamu athari zake kwa mazingira na viumbe hai..

"Kwa sasa nimepisha eneo hilo baada ya kutembelewa na viongozi wa mtaa na kunipa maelekezo kuwa natakiwa kuondoa mazao yangu ili kulinda chanzo cha maji kiwe salama," alisema Thomas.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 29, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## Bagamoyo yawaengua 'wala unga' 744, wanalishwa dawa warudie ubinadamu



Ukurasa 12

## Asimulia mara tatu alivyochungulia vifo Ziwa Victoria, wenzake yawafika

# Mkuu Ngorongoro aorodhesha ushindi wao kimazingira, chanda na pete na zama Samia

**Na Mwandishi Wetu**

WASTANI wiki tatu zijazo, chereko zitamea kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kusherehekea miaka mitatu kwa aliyoyapanga na kuyarithi kimajukumu, kutoka kwa mtangulizi, Dk. John Magufuli, yeye akiwa Makamu Rais.

Wengi wanafurahia, kila mmoja na aina ya kicheko kama la kukamilika shauku ya umeme kamili kutoka Bwawa la Umeme Mwalimu Nyerere.

Hapo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorogoro (NCAA), nayo mapema hata kabla tarehe kufika chereko ya mwaka wa tatu, inajivunia mafanikio ya uongozi wa Rais Dk. Samia.

Mojawapo inalolitaja katika tafsiri ya kimazingira, ni kufanikisha kuwahamisha wakazi kwa hiyari, kuhuisha ustawi wa mazingira na ardhi, mchakato aliyouanzisha Rais Machi mwaka 2022, kundi la wakazi likakubali kuhama kwenda kwenye baadhi ya mikoa Jirani.

Kamshina Mkuu wa NCAA, Richard Kiza anasema

kaya 23,889 zenye watu zaidi 100,000 na mifugo zaidi ya 850,000 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, zimekuwa katika changamoto zaidi ya miaka 60, tangu kuanzishwa NCAA. Sababu kuu ni mwingiliano wa shughuli za uhifadhi na utalii.

Kamishna Kiza anasema, Hifadhi ya Ngorongoro ilianzishwa mwaka 1959, kwa kuigawa Hifadhi ya Taifa Serengeti; sasa Ngorongoro ina kilomita za mraba 8,292.



Watalii wakishangaa maajabu ya Ngorongoro. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

"Hifadhi hii ilianzishwa kwa ajili ya matumizi mseto ya ardhi ambao mambo yanafanyika kwa pamoja, kama kuendeleza uhifadhi wa maliasili na malikale; kusimamia maendeleo ya jamii ya watu wanaoishi ndani ya mamlaka yaani Hadzabe, Masai na Datoga," anasema.

Kamishna Kiza anasema serikali baada ya kupitia utafiti kuhusu matumizi mseto ya ardhi ya eneo la hifadhi, ilichukua uamuzi wa busara kuwaelimisha wakazi wa NCAA kuhama hiari maeneo mengine yaliyotengwa.

Hapo akafafanua, mwananchi wakapewa fursa kuamua kuhama kwa hiari kupisha uhifadhi na wakiboreshewa maisha yao, kutengewa pa kuhamia; mkoani Tanga katika kijiji cha Msomera, wilayani Handeni na Saunyi, wilaya Kilindi; vilevile kijijini Kitwai B na wilaya ya Simanjiro, Manyara.

Anasema wananchi hao walipwa fidia kisheria na ziada ya motisha, akifafanua: "Malipo ya kisheria zinajumuisha fidia ya maendeleo, gharama ya usafiri wa watu na mali zao.

"Malipo ya motisha (malipo yasiyo ya kisheria) yanajumuisha nyumba moja katika eneo lenye ukubwa wa ekari mbili na nusu kwa kila mkuu wa kaya, shamba lenye ukubwa wa ekari tano kwa kila mkuu wa kaya pamoja na hati miliki ya kiwanja na shamba pamoja na eneo la malisho ya mifugo."

Anafafanua motisha; shilingi milioni 10 kwa kila mkuu wa kaya, chakula kwa miezi mitatu na malazi eneo la Karatu, wakati wa kusafiri.

"Kwa wale wanaoenda maeneo waliyochagua wenyewe wanapewa malipo sawa na wengine isipokuwa motisha inakuwa shilingi milioni 15 badala ya milioni 10," anasema Kiza.

**SURA YA MIPANGO**

Kamishna Kiza anasema, uamuzi huo inayobebwa na mipango ya Rais, umeongeza hamasa kwa wananchi kujenga imani na serikali kuboresha maisha yao.

Mradi huo awamu ya kwanza, ulianza Juni, mwaka 2021, Rais Dk. Samia akiwa na miezi mitatu madarakani kwa kuanza ujenzi wa nyumba 503 na nyingine kijamii, zikiwamo shule, miundombinu maji, zahanati, barabara, mawasiliano, umeme, majosho, mabwawa, malisho na huduma posta.

Hadi kufika Januari mwaka jana, mkakati awamu ya kwanza ulikamilika, kaya 551 zenye watu 3,010 na mifugo 15,521 zilihamia Msomera, Handeni.

Awamu ya Pili ikaanza Julai mwaka jana kwa ujenzi wa nyumba 5,000, kati ya hizo Msomela nyumba 2,500, Saunyi 1,000 Kilindi na Kitwai 'B', Simanjiro nyumba 1,500.

Pia, Kamishna Kiza anafafanua hadi kufikia Februari 25 mwaka huu, kaya zilizohama kwa hiari kutoka Ngorongoro ziko 1,042 zenye watu 6,461 na mifugo ipatayo 29,919. "Idadi hii ya watu na mifugo ni kwa awamu zote mbili ya kwanza na ya pili, "anasema.

**CHAKULA KWA JAMII**

Kamishna Kiza anasema NCAA imekuwa ikigawa unga, sukari na siagi kwa ajili ya uji kwa shule 27 za msingi zilizomo ndani eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Anasema kati ya mwaka 2021 na 2024, NCAA iligawa kilo za unga 32,620, kilo 11,350 za sukari na kilo 3,100 za siagi kwa shule hizo.

Katika kuboresha ustawi wa maisha ya wakazi wa eneo la Ngorongoro, anasema mamlaka imekuwa ikinunua na kugawa mahindi kwa bei yenye punguzo kwa wenyeji.

Mpaka kufikia Januari mwaka huu, tani 600 zimegawiwa kwa wakazi wainaoishi ndani ya hifadhi hiyo. Anasema wakati Dk. Samia anaingia madarakani, alikuta sekta ya utalii ikiyumba na kwa juhudi zake binafsi, Novemba mwaka 2022, Rais akafanya ziara kikazi China, alikopata shilingi bilioni 25.

Ni pesa za kuendeleza Ngorongoro Lengai, UNESCO Geopark na miundombinu mingine ya utalii ikiwamo nyumba ya Makumbusho itakayojegwa katika lango kuu la kuingilia Ngorongoro (Lodoare).

Kiza anasema NCAA imeendelea kusimamia na kudumisha hadhi yake kimataifa kutambuliwa kama 'eneo lenye urithi mchanganyiko wa maliasili na malikale', na uwapo wa miamba na sura za nchi zinazoelezea dunia ilivyojiumba na kuwa moja ya maajabu saba ya dunia.

MAZINGIRA

UVUVI UNAVYOSHIKAMANA NA MAUTI...

# Asimulia mara tatu alivyochungulia vifo Ziwa Victoria, wenzake yawafika

## •Kisa? Vifaa na elimu duni, ushirikina, ulevi, hali hewa..

**Na Christina Mwakangale,**
aliyekuwa MWANZA



"NIMEPONA mara tatu kufa maji. Nimeshuhudia wenzangu kutoka katika mtumbwi tuliyomo wakizama na kufa haikuwa dhamira yangu, ila nilishindwa kumuokoa."

Ni simulizi zake Nipashe ilipokuwa jijini humo, huku Shirika la Afya Duniani (WHO) katika ripoti ya mwaka jana inataja takribani watu 236,000 wanaokufa maji duniani kila mwaka, ikishika nafasi ya tatu katika vifo vya ajali.

Inaelezwa hadi sasa asilimia 90 ya vifo vinatokea katika nchi zenye uchumi mdogo na kati, utafiti wa Shirika la Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo ya Uchumi (EMEDO) Tanzania, Septemba 2021 katika mikoa mitatu ya Kanda Ziwa ikiibatiza 'Mtazamo na Hatari ya Kuzama Ziwa Victoria; Mara, Mwanza na Kagera'.

Inatajwa kukosekana stadi na vifaa duni kama makoti na vyombo vya kuzuia kuzama, utumiaji vilevi kama bangi, imani potofu, elimu na usimamizi duni wa kanuni, vyote ni vyanzo vya ajali majini.

Aidha, Jumuiya ya Wavuvi wa Mwambao wa Ziwa Victoria, inaeleza wastani wa wavuvi 217 kati ya 100,000 hupoteza maisha kila mwaka majini.

Kwa mujibu wa Tovuti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ni sekta iliyochangia ukuaji uchumi na kuondoa umasikini. Mwaka 2021, ikichangia asilimia 1.8 katika Pato la Taifa,Ikiwa asilimia 2.5 katika mwaka 2020/2021 na kutoa ajira za moja kwa moja 194,804 wakati huo.

### YALIYOMKUTA MVUVI

Mvuvi Morrison, mzaliwa wa mkoani Mara, sasa mkazi wa jijini Mwanza akiwa baba wa familia ya watoto tisa, ofisini kwake ni Victoria. Anakiri ni ajira iliyozingirwa na hatari, hatamani mwanawe yeyote afuate nyayo zake.

"Nimefanya kazi ya uvuvi tangu mwaka 1995. Kazi ya uvuvi wengi tunafanya kwa sababu ya shida ya kutafuta tu kipato, ila ni hatari kwa dakika chache tu unaweza kupoteza maisha," anasema.

Hapo ni kauli fupi inayoiacha Nipashe katika maswali, mwenyewe akiifafanua: "Life jacket original' (koti halisi la kuzuia kuzama) lina gharama linauzwa Sh. 50,000. Sasa kwa sisi wavuvi wadogo, hapa Sweya (Mwanza), hiyo ni fedha nyingi...

"Kwa kweli unakuwa unatembea (ziwani) tu na 'roho mkononi'. Hatutumii makoti hayo, wengi kwa ujumla. Tulijaribu kuwaomba (maofisa uvuvi) watutafutie makoti hayo hata kwa mkopo, ila wao wakija (maofisa) wanadai tu leseni wanaondoka!"

Analalama: "Wanaangalia pesa, ila kuangalia usalama wetu hakuna! Mvuvi unapata Sh. 100,000 kwa mwaka, unaigawaje? Unafika nyumbani kwa siku labda una Sh.10,000 unaigawaje?

"Bado nyumba umepanga na inawezekana usiku kucha hujapata kitu, shule watoto na matumizi mengine. Ndio maana ajali kwa wavuvi wadogo ni nyingi, haziishi. Unapokumbana na dhoruba kila mtu anajiokoa kivyake.

"Mfano usiku na wengi uvuvi ni usiku. Kutoka nchi kavu ziwani hadi unapovua ni takribani saa tatu au nne, kwa hiyo maana yake kuna kina kirefu. Ikitokea lolote hujui kuogelea, chombo unachotumia duni, huna koti, dakika chache tu umepotea, unazama kama jiwe lililorushwa majini.

"Kazi hii wengi hawajui kuogelea hata mita tatu, tunafanya tu hii kazi kwa sababu ya shida. Ajali ni muda wowote"

### CHUPUCHUPU TATU MAJINI

"(Tukio la kwanza 2003) mwaka 2013 na 2017 tukio lilijirudia tena. Ni tamaa zetu tu wavuvi siku hiyo Mungu kweli alijalia tulipata mzigo mkubwa...

"Mmoja anasema hatuwezi kumwaga samaki, mwingine anasema, dakika chache tulizama," anatamka Morris Obunga (54), mkazi wa Mtaa wa Sweya, Nyegezi, jijini Mwanza, vyote vikimuingiza katika rekodi alivyopona chupuchupu, kupoteza uhai wake ziwani.

Anaanzisha orodha yake kwamba mara ya kwanza mwaka 2003 akiwa na wenziwe wawili, pekee alikuwa na stadi ya kuogelea.

"Tukio lilitokea karibu na kisiwa cha Kayenze, nahodha aliyekuwa anaendesha chombo alishindwa kuongoza, sababu ya upepo. Tulikuwa wanne, mmoja wetu alizama, alipoteza maisha. Eneo hili tulizama tangu saa mbili asubuhi kuja kuokolewa saa tisa alasiri.

Anakumbusha jitihada zako kijinusuru majini hatari ilipojiri, akisimulia; "Nikawaambia 'ruka kwenye maji' ili nigeuze chombo kumwaga mzigo na maji.

"Ni dakika chache tu, nilipokibinua chombo, nikaanza kufuata mmoja kumleta kwenye mtumbwi. Mimi sijasomea kuogelea ila nina ujasiri ninaweza kuogelea kwa saa nyingi."

Morrison anaendeleza simulizi za kumuokoa mwenzake "Nilipomfuta nikaona kama namshindwa, shida ya maji mtu anayetapatapa kwenye maji ukifanya masihara unazama naye.

"Ukimshika vibaya anakwenda na wewe, nikang'ang'ana mara kadhaa, nikashindwa. Nikaona bora niachane naye hapa na mimi nitakwenda. Ila haikuwa dhamira yangu..."

Hapo Nipashe ikamuona mtoa simulizi huyo akipumzika dakika kadhaa akizama katika simanzi kurejea kumbukumbu zao ya mkasa huo, akifafanua hatua iliyofuata:

"Nikaogelea nikarudi kwenye chombo. Kwa hiyo tulipona wawili. Lakini tungekuwa na 'life jacket' ingesaidia hata kama mtu hajui kuogelea ataelewa kwa saa zaidi ya sita. Koti ukivaa aidha utaletwa kwenye mwalo au wavuvi watakukuta, wakuokoe."

Morrison anakumbuka mkasa mwingine miaka 10 baadaye, 2013 akieleza:" Mungu alitujalia tulipata samaki wengi, lakini sasa tamaa zetu wavuvi, ubebe vyote ziwani, utaweza! Mzigo ulikuwa mkubwa, mwenzetu mmoja akasema hatuwezi kumwaga samaki.

"Tukaanza kuondoka, upepo, mawingu...tulianza kuzama, hakuna alifariki. Niligeuza chombo na kumwaga mzigo wote, wenzetu wakaja kutuokoa, hatukuwa na 'life jacket'."

Pia, anadodosa mkasa wa tatu tatu kwamba: "Tulizama, nikamwokoa mmoja hadi kando ya Ziwa, kwa sababu tukio lilitokea si mbali sana na nchi kavu. Tukaita wenzetu, chombo kikapotea na mzigo."

Siri inayomnusuru katika majanga yote matatu, anataja uzoefu wake wake kuogelea, akisema imempa wasifu kushirikishwa katika uokoaji, ajali za kawaida na kitaifa.

"Nakumbuka ilipotokea ajali ya MV Bukoba (1996), niliitwa kuokoa watu. Nina kipaji cha kuogelea kwa saa nyingi, ila si kuzamia. Wengi hawakuwa na 'life jacket' ukiwa na koti hili unaweza kukaa majini kwa saa sita hadi 12," anasema.

### AKATAA KURITHIWA

Morrison anasema, watoto wake sita wa kike na wanaume watatu, aliyeonesha dalili kufuata nyayo zake. "Mungu alijalia nikapata watoto wengi wa kike, watano wameshaolewa. Wa kiume ni watatu.

"Kijana mmoja nikambadilishia kazi, alipomaliza darasa la saba hakufanya vizuri, nikasema asiegemee sana kwenye uvuvi, nikampeleka kwenye ufundi katika gereji huko," anafafanua.

### JICHO LA SERIKALI

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga Wizara ya Afya, Dk. Ntuli Kapologwe, Novemba mwaka jana akiwa Dar es Salaam akalitolea neno suala hilo kwenye ufunguzi wa Mpango wa Kitaifa kujadili kuzuia Kuzama Majini nchini.

Anataja takwimu za wanaoathirika zaidi ni watoto na vijana, huku zaidi ya asilimia 90 ya vifo vinatokea katika nchi zenye vipato vyaa chini na kati.

"Suala la kuzama maji ni tatizo linaloathiri jamii yetu na kuwa tishio kwa maisha ya watu hususan watoto, wavuvi, wasafiri wanaotumia usafiri wa maji na hata wale wanaoishi karibu na fukwe," akisema vinaongezeka kwa kasi, akitaka jamii kuchukua hatua.

Dk. Kapologwe anasema, kuzama maji kunazuilika kupitia hatua za kiusalama kwa wahusiska maji kama vile wavuvi, ikiwamo kupatiwa elimu ya hatari na mafunzo kujiokoai.

"Lazima kuendeleza programu za kuzuia kuzama maji kulingana na mapendekezo ya WHO, unaosisitiza uwekezaji vizuizi, usimamizi, ujuzi wa kuogelea,

INAENDELEA UK. 13

AFYA

# Bagamoyo yawaengua 'wala unga' 744, wanalishwa dawa warudie ubinadamu

## • Wamehamasishwa wakajitokeza; wanane wamehitimu

**Na Sabato Kasika**

WILAYA ya Bagamoyo mkoani Pwani imetangaza ushindi kwa kuachana na uraibu wa kutumia dawa za kulevya na sasa wanahudhuria kliniki katika hospitali ya wilaya hiyo, kupata tiba, ikiwamo dawa za methadone.

Matumizi ya dawa za kulevya ni miongoni mwa changamoto kubwa inayowakabili vijana, maeneo mbalimbali nchini na kusababisha kuwa tegemezi, badala ya wazalishaji mali.

Husna Kipilipili, ni Mratibu wa Afya ya Akili na Tiba ya Dawa za Kulevya wa hospitali hiyo, anayetoa maelezo hayo wiki iliyopita, katika mkutano wa uhamasishaji wa afya bora, kwa waraibu wa dawa hizo, unaotekelezwa na shirika la Life & Hope Rehabilitation Organisation (LHRO).

Anasema mwaka 2020 walifanya kazi ya utambuzi wa vijiwe vya watumiaji wa dawa hizo na kubaini vipo 11 wilayani humo, vikiwa na jumla ya watumiaji 300, nane kati yao wameweza kuacha dawa hizo.

Hata hivyo, baada ya kutolewa elimu baadhi waliokuwa mafichoni nao wakajitokeza hata idadi ikaongozeka maradufu watumia 'unga' waliokuwa mafichono wakajitokeza.

"Kulikuwa na changamoto, kwani wauza dawa wana mbinu za kuficha watumiaji ili biashara ya kuuza dawa iendelee. Wakati huo, tulifanikiwa kupata vijana nane walioacha dawa hizo na kuanza kupata huduma ya methadone," anasema Husna.



Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete (katikati), akifuatilia kinachoendelea katika maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani katika Viwanja vya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA), Juni 26, 2016. **PICHA: MTANDAO.**

Anafafanua, kadri miaka inavyokwenda, ndivyo elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya inazidi kuenea na kwamba hadi Februari 21 mwaka huu, kuna vijana 744 wanaofika hospitali ya wilaya kunywa dawa tiba za methadone.

"Hii ni hatua nzuri, ambayo inasaidia vijana kurudi katika hali ya kawaida kwa kuimarika kwa afya zao ili waweze kuwa wazalishaji mali katika familia zao badala ya kuwa tegemezi," anasema.

Husna anasema bado kuna kundi kubwa la vijana wanaotumia dawa hizo hawajafikiwa, ili kuwaondoa katika hatari hiyo.

"Hivyo tuna mpango wa kuzungukia tena, kwa ajili ya kufanya utambuzi wa maskani zao kwa lengo la kuwaibua wengine zaidi, ili kuwaondoa katika uraibu wa dawa za kulevya," anasema.

**HATUA ZAIDI**

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika linalohudumia waraibu wa dawa za kulevya la Life & Hope Rehabilitation Organisation (LHRO), Al-Karim Bhanji, anasema wanaendesha mradi wa kuwakomboa waraibu.

Anafafanua kuwa mradi huo unaendeshwa katika kata tano za Dunda, Magomeni, Nianjema, Kisutu, na Kiromo, ukilenga pia kuwafanya waraibu kutambua haki zao za msingi.

Bhanji anashauri kuwapo kwa mikakati itakayowawezesha kiuchumi vijana wanaochana na matumizi ya dawa hizo, ili wasijikute wakirudi kwenye uraibu.

Anataja baadhi ya mikakati hiyo kuwa ni kuwapa elimu ya ujasiriamali, pia mitaji wawe na shughuli za kufanya kwa ajili ya kujiingizia kipato wamudu gharama za maisha. "Vijana ni nguvu kazi ya taifa na hapa tunaelezwa kuwa 744 wameacha dawa za kulevya, hii ni hatua nzuri, lakini ni vyema kukawa na mikakati ya kuwawezesha kiuchumi," anasema.

Anafafanua kuwa suala la vijana kuacha dawa za kulevya na kuendelea kuishi katika mazingira ya awali yaliyosababishia hali hiyo huku wakiwa hawana shughuli ya kufanya, wanaweza kurudi katika uraibu.

"Wakirudi katika uraibu, hawawezi kuwa msaada kwa familia, badala yake wanachangia kuingiza hasara kwa kusababu wanalishwa tu na wakati mwingine kuiba vitu vya nyumbani na kwenda kuuza," anasema.

Bhanji anafafanua kwamba, katika jamii shughuli za kufanya zipo nyingi, zinazoweza kuwaingizia vijana kipato, kikiwamo kilimo cha bustani na kuacha na kwamba ni wakati sasa wawawekea mazingira ya kujishughulisha.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya hiyo, Dk. Kandi Lussingu, anawashukuru viongozi wa idara ya maendeleo ya jamii, polisi kata, dawati la jinsia na wadau wengine wanavyoshirikiana kuwatoa vijana katika uraibu wa dawa za kulevya.

"Kuwaondoa vijana katika uraibu wa dawa za kulevya ni hatua moja ya muhimu, hivyo tuendelee kushirikiana ili kuokoa kizazi kijacho, kwani ndio nguvu kazi ya taifa la kesho," anasema Dk. Kandi.

Anasema, ushirikiano huo uendelee kwa shirika la LHRO, ambalo limejitosa kutoa elimu kwa ajili ya kusaidia waraibu, wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kutambua haki za kila upande.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo, OCD Mushana Mujema, anasema kitendo cha Mkurugenzi wa shirika hilo kuhusisha polisi katika mradi huo, ni ishara ya kutaka kusaidia vijana kutoka katika maisha ya uraibu.

"Kazi yetu ni kuzuia vitendo vyote vya uhalifu, kwa kuwa baadhi ya vijana wanaotumia dawa hizo hujihusisha na vitendo hivyo, tuko tayari kutoa ushirikiano ili kusaidia vijana wetu kuondokana na maisha yao ili wawe msaada kwa familia, jamii na taifa kwa jumla," anasema Mujema.

# Asimulia mara tatu alivyochungulia vifo Ziwa Victoria...

**Inatoka Uk. 12**

mafunzo ya uokoaji pamoja na kudhibiti usafiri majini.

**MTAALAMU WHO**

Mtaalamu wa WHO, David Meddings, anawaambia waandishi wa habari kuna utafiti kimataifa uitwao: 'Global Report on Drowning: Preventing a Leading Killer-2014', uliobaini watu 372,000 hufa kwa kuzama maji.

Meddings, Mhariri Mkuu katika ripoti hiyo, anaeleza "Idadi hii ya vifo ni karibu theluthi mbili ya ile ya utapiamlo na zaidi ya nusu ya ile ya malaria... hakuna juhudi pana zinazolenga kuzia kuzama, zaidi ya nusu ya waliojeruhiwa ni wenye umri wa chini ya miaka 25."

**MRADI VICTORIA**

Mratibu wa Mradi wa Kuzuia Watu Kuzama Maji katika Ziwa Victoria, Arthur Mugema, anasema ndiko kwenye mwambao wa nchi kavu takribani maili 2,000 linakitegemea na wavuvi wapatao 110,000 nchini.

Anasema samaki wanaovuliwa humo huuzwa Afrika Mashariki na kimataifa, lakini wanavua wengi wamo hatarini kuzama kutokana na mapungufu yao, ikiwamo vifaa duni.

"Tanzania ina sera na miongozo kuhusu usalama wa maji kwa wavuvi, wasafiri, usafirishaji, mamlaka za hali ya hewa ila kuna changamoto za utekelezaji wa kanuni.

"Utafiti huu katika mikoa mitatu; Mara, Kagera na Mwanza, ulihusisha jamii ya wavuvi. Mkoani Mwanza tulihusisha wakazi wa Sweya, Wila ya Nyamagana. BMU (Beach Management Unit) wanatakiwa kuwa 15 angalau watatu wawe wanawake.

"Watengeneza boti wanawajibika kutengeneza na kufanyika matengenezo boti, ingawa wanasema wamerithi kazi hiyo kutoka kwa wazazi wao, hawana ujuzi rasmi. Usimamizi wa miongozo ni duni," anasema Mugema.

Kadhalika, anasema utafiti ulibaini wavuvi wanatumia simu za mkononi, ingawa upatikanaji wa mtandao ni mdogo wawapo ziwani, hata kuwa chanzo cha kukosa mawasiliano wanapohitaji msaada.

"Hata kama 'life jackets' yangeuzwa kwa bei nafuu au kugaiwa na wamiliki wa boti, wavuvi wengi hawako tayari kuvaa. Umuhimu wa makoti hayo ni duni. Huko Sweya, elimu ni duni ya usalama na kuzama, wavuvi wengine huyauza makoti na wakirudi kwa wamiliki hugoma kununua makoti mengine," anasema.

"Makoti yenye ubora huuzwa kati ya Sh. 70,000 hadi 100,000 (Dola 30.10- 43.00). Wamiliki wa boti wanadai wavuvi hawako makini, ili kuyatunza makoti hayo.

"Inachukua asilimia 60 ya vipande vya mbao kukamilisha boti la wastani boti na mbao ngumu huuzwa kati ya Sh. 20,000 hadi 37,000 (Dola tisa hadi 16) au Sh. 8,000 hadi 12,000 kwa mbao ya kawaida. Maboto mengi hudumu kwa miezi saba hadi 12 kabla ya kuanza kukarabatiwa sana.

Mugema anasema utafiti pia ulibaini kuwapo imani potofu. "Jamii zilizohusika katika utafiti huu, ushirikina ulihusika moja kwa moja na ujenzi wa vyombo vya majini. Wavuvi wakikumbana na upepo mkali ziwani wanaamini ni ushirikina.

"Hawachukui tahadhari. Huko Irondo, walisema kwamba kukiwa na upepo mkali, mmoja wao katika boti atajikata sehemu ndogo ya kidole na kudondosha matone ya damu, dhoruba itakoma," anasema.

Mugema anasema, walibaini matumizi ya vilevi, kuwapo ushuhuda wa mvuvi mwendesha boti alizama na baadae waligundua alikuwa amelewa.

MAZINGIRA

# Ushuhuda wa harakati zake DUWASA kufuta shida maji Dodoma 'iwe isiwe'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUNA usemi 'Maji ni Uhai'. Ni bidhaa ya kila kiumbe, binadamu, viumbe vingine na mimea duniani.

Umuhimu wake unadhihirika kwa wanasayansi, wanaeleza sehemu kubwa ya mwili wa binadamu ni maji na bila maji hakuna maisha.

Nyumbani hakuna kitakachopikwa kwa kuwa chakula kuiva kinahitaji maji, hakuna atakayeoga, wala kufanya kazi pasipo kula.

Katika kutambua umuhimu wa maji, serikali kimuundo imeanzisha mamlaka mbalimbali za maji. Hapo ndipo inapatikana Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Dodoma (DUWASA), iliyoanzishwa mwaka 1998.

Hapo, kama yalivyo mamlaka mengine, imepewa jukumu la kuhakikisha inatoa huduma bora na endelevu ya usambazaji majisafi na safi kwa mazingira ya wakazi wa Dodoma.

Mwezi Juni, 2017, serikali ilitangaza azma yake ya kuhamia Dodoma na tathimini iliyofanyika hivi karibuni inaonyesha kuwa, mahitaji ya maji mjini Dodoma hadi kufika mwaka 2022, ni lita za ujazo milioni 133.4 kwa siku.

Hali kadhalika, tuendako mwaka 2026 inatarajiwa kuwa lita 146,317,000 kwa siku; mwaka 2036) kufika, lita 204,315,000 kwa siku; na mwaka 2051 kufika lita 417,308,000.

Kutokana na mahitaji hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, anaeleza mikakati mbalimbali ya mamlaka hiyo, akisema DUWASA imejipanga kuhakikisha Dodoma inakuwa na maji ya uhakika kwa wakazi na watumishi wanaohamia.

**VYANZO MAJI**

Mhandisi Joseph anasema, chanzo kikuu cha maji kwa wakazi wa Dodoma, ni visima virefu vilivyochimbwa katika bonde la Makutupora, eneo la Mzakwe, kukitarajiwa miundombinu hiyo kuzalisha lita milioni 61.5 kwa siku, hata ikasafirishwa hadi kulikolengwa.

Aidha, anataja vyanzo vingine vidogo kwa maeneo mahsusi ambavyo ni; Nzuguni, Ihumwa kwa ajili ya Mji wa Serikali, Iyumbu kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Kata ya Iyumbu, Hospitali ya Benjamin Mkapa na Kata ya Nghong'onha, ambavyo kwa pamoja vinazalisha lita 17.1 milioni kwa siku.



Tanki la maji katika mradi ulioko Nzuguni, Jijini Dodoma. Picha nyingine, pilika za shughuli za mradi wa maji jijini Dodoma. **PICHA ZOTE: AGUSTA NJOJI.**



"Vyanzo vyote hivyo na vingine vidogovidogo vinafanya uzalishaji kuwa jumla ya lita milioni 78.6 kwa siku, wakati mahitaji ya sasa (2022) ni lita milioni 133.4 kwa siku.

"Hivyo upungufu wa maji katika mji wa Dodoma ni lita milioni 54.8 kwa siku. Upungufu huu unaongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko la watu na shughuli za kiuchumi na kijamii katika jiji la Dodoma," anasema.

**UTEKELEZAJI MIRADI**

Mhandisi Joseph, anafafanua kwa sasa kuna miradi kadhaa inayotekelezwa kuimarisha upatikanaji wa majisafi.

"DUWASA tunashukuru serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuipa kipaumbele DUWASA katika kutatua changamoto za upatikanaji wa maji na uondoshaji majitaka mjini Dodoma na Miji ya pembezoni," anasema

Anataja kuwa ni Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria, utakaohusisha ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, matenki, vituo vya kusukuma maji, na mabomba ya kusafirisha maji kutoka Mwanza mpaka Dodoma.

"Wizara ya Maji imeshatangaza zabuni ya Mhandishi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu, zabuni za mkandarasi wa ujenzi, pamoja na kusimamia utekelezaji wa mradi huu. Wizara ipo katika hatua za mwisho kusaini mkataba na Mhandisi Mshauri," anasema.

Lingine anataja ni Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Farkwa, utakaonufaisha wakazi wa Dodoma Mjini; Chemba, Bahi na Chamwino Mjini, lengo ni kujitosheleza mahitaji ya maji hadi mwaka 2038.

Anasema Bwawa la Farkwa, litajengwa katika kijiji cha Mombose, wilayani Chemba, Dodoma na mradi utahusisha ujenzi wa bwawa, chujio la maji, matenki ya kupokea maji na ujenzi wa bomba kuu kutoka Farkwa hadi Dodoma linalokadiriwa kuwa na urefu wa kilomita 117.

Anasema, bomba hilo litakuwa na matoleo ya kugawa maji kwa vijiji vyote vilivyopo ndani ya umbali wa kilomita 12 pande zote za bomba hilo katika Wilaya za Chemba, Chamwino, Bahi na Dodoma.

"Mradi huu unakadiriwa kugharimu takribani Dola za Kimarekani milioni 135.8 sawa na shilingi bilioni 312.08 katika awamu ya kwanza.

"Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeshatenga fedha hizo kutekeleza awamu hii. Miongoni mwa hatua zilizofikiwa ni utiaji wa saini wa mkataba kati ya Wizara ya Maji na Mhandisi Mshauri wa kurejea usanifu wa awali... mnamo tarehe 23 Oktoba, 2023," anasema.

Kuhusu uchimbaji wa visima 10 pembezoni mwa mji ili kupata vyanzo vingine vya maji kwa wakazi wa Jiji la Dodoma, anasema DUWASA imeingia Mkataba na kampuni ya PNR Drilling Company, itakayochimba visima katika maeneo mbalimbali ya pembezoni.

Inaelezwa tayari mkandarasi ameshaanza kazi rasmi mnamo Oktoba 2023 na gharama za mradi ni shilingi milioni 403.996. Inaelezwa, kufika Disemba mwaka jana, mkandarasi alishachimba visima vitano katika maeneo ya Kilimani, Mkonze, Ntyuka, Iyumbu, na Ndachi.

Kadhalika, Mkurugenzi huyo anautaja mradi mwingine ni wa maji safi Nzuguni, unaotekelezwa katika awamu mbili; kuboresha huduma ya usambazaji maji katika katikati ya jiji la Dodoma na Kata ya Nzuguni kwa ujumla.

Hapo mtazamo unaolengwa, anautaka Mhandisi Joseph ni kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita 68,600,000 hadi 76,000,000 kwa siku, sawa na ongezeko la asilimia 11.7

Anafafanua kuwa, katika awamu ya kwanza ya mradi umefikia umefikia asilimia 96 na DUWASA inatekeleza ujenzi wa mradi huo kwa kutumia wazabuni saba na kazi zinazofanyika ni pamoja na uchimbaji na uendelezaji wa visima vinne.

Mengine anataja ni kununua transfoma sita, ujenzi wa mtandao wa kusafirisha na kusambaza maji wenye takribani kilomita saba, ujenzi wa matenki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 3.5, vibanda vya kuendeshea pampu.

Pia anataja ujenzi wa ofisi ya mradi, usimikaji wa pampu za kusukuma maji, ujenzi wa miundombinu ya umeme, ujenzi wa vifaa umeme 'fire hydrants', ufungaji mfumo kompyuta utakaofanya mfumo maji kujiendesha wenyewe, na upandaji miti.

Kwa mujibu wa Mhandisi Joseph, mradi huo una jumla ya mikataba saba yenye thamani ya shilingi bilioni 4.39 fedha zote za kutekeleza mradi huo zinatolewa na serikali.

Kuhusu awamu ya pili, anasema kuhakikisha huduma ya maji inaimarika Mjini Dodoma, DUWASA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, inachimba visima vitano na kimoja chenye kina cha mita 300 katika eneo la Nzuguni.

"Mkandarasi kampuni ya PNR Ltd ameanza kazi ya uchimbaji wa visima vitano kwa gharama ya shilingi milioni 220, eneo la Nzuguni na Mkandarasi, kampuni ya Shanxi Constrtuction atachimba kisima kirefu eneo la Nzuguni kwa gharama ya shilingi milioni 570, wakazi wapatao 75,968 katika eneo la Nzugun, na baadhi ya maeneo jirani ya Kisasa, Ilazo na Swaswa," anasema.



HABARI DODOMA

# Jiji lang'aka takataka kurundikwa mitaani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma limekuja juu na kuzionya kampuni na vikundi vya ukusanyaji taka kwenye maeneo yake na kusababisha kulundikwa mitaani badala ya kuhifadhi kwenye makontena na kuhatarisha afya za wananchi.

Mkuu wa Idara ya Usafi wa Mazingira wa Jiji hilo, Dickson Kimaro akizungumza jana baada ya kufanya ukaguzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali, alibaini makontena ambayo hayatumiki kuhifadhiwa taka na badala yake zimelundikwa chini.

"Baadhi ya makotena yaliyokabidhiwa kwenye vikundi na kampuni za usafi hawayatumii kuweka taka zao humo badala yake uchafu huo unalundikwa chini kinyume na matumizi yaliyokusudiwa.Hii inasababisha taka kusambaa na kuhatarisha afya za wananchi," alisema Kimaro.

Alisema kitendo hicho pia kimekuwa kikisababisha hasara ya mamilioni ya fedha kwa kutumia magari na mitambo kuziondoa na kuzisafirisha hadi dampo.

"Vikundi vyote vya kijamii vinatakiwa kusimamia kikamilifu na kutekelza wajibu wake kwa mujibu wa kifungu namba 73 (4) (5) (6) (7) na 76 (3) (a) cha Sheria ya Afya ya Jamii namba 1 ya mwaka 2009 kwa kwa mujibu wa makubaliano kati ya vikundi na makampuni hayo," alisema.

Mkuu huyo alizitaka kampuni na vikundi hivyo kuhakikisha taka zote zinaondolewa katika maeneo ya biashara na makazi kwa kufuata ratiba iliyopo ya mtaa na kata.

"Pia wafanyabiashara ndani ya masoko yaliyopo Jiji la Dodoma wahakikishe wanafanya usafi kwenye maeneo yao ili kuyaweka mazingira yao katika hali ya safi ikiwa na kuepukana na magonjwa yanayotokana na uchafu hasa kipindi cha mvua," alisema.

Kwa mujibu wa Kimaro, miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa dhidi yao ni kutozwa faini isiyopungua Sh. 300,000, kuondoa taka na kunyang'anywa makotena hayo ili wapewe watu wenye uwezo wa kulifanya Jiji kuwa safi.



Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonaz (kulia), akibadilishana hati na Mkurugenzi wa kampuni ya DMG, Rayton Kwembe jijini Dodoma juzi, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa ujenzi wa meli za uvuvi na kilimo bahari kuu, itakayoendana sambamba na ujenzi wa viwanda vya kuchakata samaki. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Meli za uvuvi kujengwa kwa mabilioni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kujenga meli nane za uvuvi wa bahari kuu kwa gharama ya Sh. Bilioni 30 kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi nchini.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonaz alitangaza mpango huo juzi kwenye hafla ya utiaji saini mikataba ya upembuzi yakinifu wa meli hizo na ujenzi wa viwanda viwili vya kuchakata samaki katika maeneo ya Kilwa na Fungurefu kupitia programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi utakaogharimu Sh. Milioni 348.

Dk. Yonaz alizitaka kampuni zilizosaini mkataba huo ya DMG na TANSHEQ kukamilisha upembuzi huo ndani ya siku 45 kwa ufanisi.

"Programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi ni moja ya programu za kitaifa za kimkakati zilizo katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano kuanzia 2021/22 mpaka 2025/26, " alisema na kuongeza kuwa:

"Lengo ni kuimarisha uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa na kuendeleza uchumi wa buluu."

Alisema kukamilika kwa upembuzi huo kutawezesha serikali kuanza ujenzi wa meli hizo ambayo unatarajiwa kukamilika mwezi ujao na viwanda hivyo.

Mratibu wa Programu ya AFDP Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu, Salimu Mwinjaka, alisema matarajio ya programu hiyo ni kuwanufaisha watu takribani milioni 1.3, ikiwamo kaya za wakulima wadogo 200,000 kupata mbegu bora za mahindi, alizeti na maharage.

Alisema vilevile itawanufaisha wazalishaji wadogo, kati wa mbegu na wafanyabiashara za pembejeo za kilimo takribani 1,000 kwa kupata mbegu bora na mafunzo.

" Wavuvi wadogo na wafanyabiashara wa samaki takribani 48,000 pamoja na wafugaji wa samaki na viumbe maji na mwani 21,000 watanufaika," alisema.

Alisema meli hizo, nne ni Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na nyingine za Shirika la Uvuvi Zanzibar (ZAFICO).

# Wasajili wa mabaraza wapewa rungu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WASAJILI wa mabaraza ya wataalam na Bodi ya Washauri katika sekta ya afya nchini wameagizwa kuweka mfumo wa kuwabaini na kuwachukulia hatua wataalamu wanaokiuka maadili ya utendaji kazi wao.

Agizo hilo lilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu katika kikao na wasajili hao cha kujadili namna ya kuboresha huduma kwa wananchi.

Dk. Jingu, alisema ni muhimu kulinda maadili ya utendaji wa kazi zao ili Watanzania wapate huduma bora za afya.

Alisema kuna kesi nyingi zinatokea katika maeneo ya kazi ambako kuna wanataaluma, wasajili na wasimamizi wa bodi na mabaraza ambao wanatakiwa kuwatembelea kufahamu kero zinazowakabili na si kusubiri kesi kwenye mabaraza yao wakiwa ofisini.

"Nendeni mkatembelee wataalamu katika maeneo yao ya kazi mkaone wanavyofanya kazi, msijifungie ofisini na msiwe mahakimu wa kusubiri hadi matatizo yatokee ndio mchukue hatua," alisema.

Alionya kuwa mtaalamu atakayebainika kukiuka maadili atachukuliwa hatua ili asiharibu taaluma na wananchi kupata huduma bora.

"Twendeni tukawajulishe wananchi juu ya sisi ni wakina nani, majukumu yetu ni yapi na njia na mawasiliano wanayoweza kutumia ili kufikia, pia msicheleweshe mashauri ambayo yanaletwa kwenye mabaraza yenu. Ongezeni ufanisi kutatua changamoto za wananchi kwa muda mfupi," alisema.

Awali Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu, alisema ofisi yake ina jukumu la kusimamia mabaraza nane ya kitaaluma, weledi na maadili ya wataalamu na Bodi ya Maabara Binafsi (PHLB) na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi (PHAB) zenye jukumu la kumshauri waziri juu ubora wa huduma na kusajili maabara na hospitali binafsi.



# CHADEMA kuwaburuta kortini viongozi vijiji kwa utapeli

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mkoani hapa kimesema kinaandaa wanasheria kwa ajili ya kuwafungulia mashitaka kortini watendaji na wenyeviti wa vijiji kwa kuwakamata wananchi na kuwatoza faini bila kuwapa stakabadhi halali na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Akizungumza baada ya mkutano wa uchaguzi, Katibu wa CHADEMA wa Mkoa wa Njombe, Baraka Kivambe, alisema wana stakabadhi za bandia za faini za malipo zaidi ya 50 zilizotolewa na viongozi hao wa serikali za vijiji kwa wananchi.

"Kwa tafsiri yake ili sisi tuonyeshe dira kwa wananchi, hii tunaanza nayo na hizo risiti tunapeleka kwa wanasheria wetu wa chama watashughulika nao mahakamani," alisema Kivambe.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Njombe, Seth Vegulla, alisema mambo hayo yanafanywa na viongozi kwa lengo la kujitengenezea ulaji.

"Serikali inaibiwa mapato ya nchi yanapotea na imekuwa sio kijiji kimoja tu ni karibu halmashauri zote za Mkoa wa Njombe," alisema Vegulla.

Alisema mwaka huu kutakuwa na uchaguzi wa serikali za mitaa na kutoa onyo kwa viongozi walioshinda kwa njia za udanganyifu kuwa watakabiliana nao, Mwenyekiti wa Baraza la Wazee CHADEMA wa Wilaya ya Njombe, Aldo Mrote, alisema anakwenda kupigania haki ya matibabu ya wazee ambao hawana bima na vitambulisho vya uzee ili wapate matibabu bure.

Mrote alifafanua kwamba wazee wengi wananyanyasika kutokana na kutokuwa na uhakika wa matibabu.

"Wenzenu tunakabiliwa na changamoto hasa matibabu, ukienda hospitali wanasema wazee wawe wa kwanza kutibiwa, lakini unakuta hakuna anayekuangalia pia upatikanaji wa dawa ni mgumu sana," alisema Mrote.

Mwenyekiti Baraza la Wanawake la chama hicho (BAWACHA) wa wilaya hiyo, Revina Wikechi, alisema katika kipindi chake cha utawala, atakuwa kipaumbele kupinga ukatili na unyanyasaji na huduma za afya.

"Niwaahidi wanawake kwamba nitakwenda kupambana na changamoto za sekta husika ikiwemo ya afya ili kuhakikisha zinapungua na wanawake na watoto wanakuwa salama," alisema Wikechi.



Baadhi ya vijana wakazi wa Tarafa ya Matamba, Halmashauri ya Makete, mkoani Njombe, wakishona viroba vyenye viazi mviringo kwa ujazo maarufu kama rumbesa juzi. Ujazo huo, unadaiwa kuwaumiza wakulima kimapato. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wahudumu watakiwa kuwatambua abiria kwenye mabasi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAHUDUMU wa mabasi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wameshauriwa kuwatambua abiria na kutoa taarifa kwenye vyombo vya usalama wanapokutana na watu wanaowatilia mashaka ili kuimarisha usalama.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa rai hiyo juzi jijini hapa kwenye mafunzo ya siku saba ya wahudumu wa mabasi ya masafa marefu yaliyoandaliwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Homera, aliwataka kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye magari yao ili kuhakikisha watu na mizigo yao iko salama na kuhakikisha hakuna mazingira hatarishi kwenye magari ikiwemo watoto kujificha kwenye sehemu za mizigo.

Alisema baadhi ya watu wasio wema, wakiwemo magaidi na wahamiaji haramu husafiri kutoka nchi moja kwenda nyingine, hivyo ni wajibu wa wahudumu hao kwa kuwa wao ni maofisa usalama namba moja kwenye gari kuwatambua na kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama ilio wakamatwe na kuchukuliwa hatua.

"Kuna siku walikamatwa watoto sita wakitokea Mbeya wamekaa kwenye buti mpaka wamefika Morogoro ile ni hatari kubwa wakipoteza maisha wenye mabasi na wewe kondakta utachukuliwa hatua kama mhalifu pia kwa sababu inawezekana umewaona na haujatoa taarifa yoyote,"alisema Homera

Kaimu Mkuu wa NIT Taaluma na Utafiti, Dk. John Mahona, alisema wanatoa mafunzo hayo kwa lengo la kuboresha huduma za mabasi ili wananchi wasafiri salama pamoja na mizigo yao na kuongeza ufanisi wa kazi kwa wahudumu hao.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Mbeya, Shaban Mbembe, alisema wanatarajia kuifanya tasinia ya wahudumu wa mabasi kuwa rasmi.

Mbembe, alisema wanashirikiana na NIT kutoa mafunzo hayo ili wahudumu hao waweze kukidhi viwango vya matakwa ya kisheria.

Alisema walianza kutoa mafunzo hayo kwa madereva na sasa wamehamia kwa wahudumu.

Alisema baada ya mafunzo hayo, watakaofuzu watawasajili na kuwapa utambulisho kuwa watoa huduma na wale ambao hawatafuzu watapaswa kupata upya ndipo waruhusiwe kufanya kazi hiyo.

# Wakulima: Wafanyabiashara wanatunyonya kwa rumbesa

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

WAKULIMA wa viazi mviringo katika Kata ya Matamba Halmashauri ya Makete mkoani Njombe wameiomba Serikali kukomesha matumizi ya vipimo visivyokuwa rasmi vinavyotumiwa na wafanyabiashara kwa madai kuwa vinatumika kuwanyonya.

Wakulima hao wamedai kuwa licha ya serikali kupiga marufuku ujazo uliozidi zaidi ya kilo 100 kwa gunia maarufu lumbesa bado kuna wafanyabiashara wanautumia huku halmashauri hiyo ikigeuza ujazo huo kuwa kitegauchumi kwa kuwatoza faini.

Mmoja wa wakulima hao, Yuston Mtweve, alisema mwaka 2023 walifanya mkutano wa wadau wa kilimo cha zao hilo na kukubaliana kitumike kipimo cha aina moja nchi nzima kwenye ununuzi, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua.

Alisema kwenye mkutano huo walikubaliana vitumike vipimo ambavyo ujazo wake hauzidi kilo 100, lakini wanunuzi wanaendelea kutumia lumbesa na kuwadidimiza kiuchumi.

Martha Mgaya, alisema wanunuzi wa viazi wamekuwa wakishona lumbesa na wanaposafirisha wanatozwa faini na halmashauri hiyo na kuzidi kuchochea kuwanyonya .

Martha, alisema wanunuzi hao wamekuwa wakifidia faini wanazotozwa na halmashauri hiyo kwa kumnyonya zaidi mkulima hali ambayo inachangia kukosa faida cha kilimo cha zao hilo.

"Sasa sisi tunaendelea kuumia kwa sababu tunatumia gharama kubwa," alisema Martha.

John Mkinga, miongoni mwa vijana wanaoshona na kupakia magunia ya viazi kwenye magari, alisema hata wao wanaumia wakati wa kupakia lumbesa kutokana na kuwa na uzito mkubwa.

Alisema wakati mwingine wanapakia viazi kwenye magari, lakini yanakwama na kulazimika kushusha na kupakia tena, jambo ambalo linawaumiza kutokana na uzito.

Mtaalamu wa Vipimo Ofisi ya Wakala wa Vipimo Mkoa wa Mbeya, Arbogast Kajungu, alisema tatizo linalosababisha iwe vigumu kukomesha vipimo hivyo ni halmashauri kugeuza ujazo huo kuwa chanzo cha mapato.

Kajungu, alisema wafanyabiashara hawaogopi kujaza lumbesa kwa sababu wanakuwa wamejiandaa kulipa faini kwenye mageti ili waruhusiwe kuendelea na safari huku wakiwa wameshawaumiza wakulima.

Aliwaomba wadau wa kilimo kushiriki kukomesha vipimo hivyo badala yake watumie visivyozidi uzito wa kilo 100 vinavyokubalika kisheria.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, William Makufwe, alisema ajenda ya kukomesha lumbesa inatakiwa kuwa ya nchi nzima badala ya kila halmashauri kuwa na utaratibu wake ili viazi vya wilaya visikose soko.

Mwaka 2022, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipiga marufuku ujazo wa lumbesa kwenye biashara ya mazao huku akiwaagiza wakuu wa mikoa na wakuu kusimamia biashara hiyo.



# Wanafunzi 9,000 wakacha masomo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema Zanzibar inakabiliwa na tatizo la utoro wa wanafunzi shuleni kutokana na takwimu kuonyesha zaidi ya wanafunzi 9,000 hawakuhudhuria masomo katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Ali Abdallah Gulamu, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah aliyetaka kujua takwimu za utoro kwa wanafunzi shuleni. Gulamu, alisema katika kipindi hicho cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2023, wanafunzi wa shule za msingi wapatao 5,952 na sekondari 3,238 waliripotiwa kutokuwa na mahudhurio mazuri shuleni kutokana na kukithiri kwa utoro.

Alizitaja baadhi ya sababu za wanafunzi hao kukithiri kwa utoro huo kuwa ni kufanya shughuli za kiuchumi na ufuatiliaji mdogo wa wazazi na walezi kwa watoto wao shuleni.

Alisema serikali imekuwa ikichukua hatua za kutatua tatizo la utoro kwa wanafunzi ikiwamo kuimarisha mazingira ya shule, kutoa chakula kwa baadhi ya shule za msingi na ugawaji wa vifaa vya ufundishaji kama madaftari na vitabu.

"Pia tumekuwa tukitoa ushauri na unasihi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili kuwafanya wasitoroke shule," alisema.

Gulamu, alisema serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango maalumu wa kuwarejesha wanafunzi waliotoroka shule na wale ambao hawakuwahi kuandikishwa kujiunga na elimu ya msingi na kidato cha kwanza.

Alisema wizara hiyo imefanikiwa kuwarejesha shuleni wanafunzi 31,639 kati ya 35,732 kuendelea na masomo katika kipindi hicho.




Mbunge wa Mfenesini, Wilaya ya Magharibi A Unguja, Zubeda Khamis Shaibu, akiangalia uzito wa mtoto aliyefikishwa katika kituo cha afya Bubwisudi alipotembelea kituo hicho, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yakamilisha ujenzi kiwanda cha kusarifu mwani

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imekamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani cha Chamanangwe Pemba na iko katika mchakato wa kuingia katika makubaliano ya uendeshaji na Kampuni ya Nutri-San ili kuliongezea thamani zao hilo na kuwanufaisha wakulima.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shabani Ali Othman wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah aliyetaka kujua jinsi SMZ ilivyojipanga kuwaondolea wakulima wa mwani changamoto ya bei ndogo katika soko la zao hilo.

Othman, alisema SMZ imeunda Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) ili kumkwamua mkulima wa zao hilo na tayari imeongeza bei ya mwani wa aina ya Spinosum kutoka wastani wa Shilingi 500 hadi kufikia wastani wa Shilingi 1,000 kwa kilo.

Alisema bei ya mwani aina ya Cottonii nayo imeongezeka kutoka Shilingi 1,200 kwa kilo hadi kufikia wastani wa Shilingi 2,000.

Alisema ZASCO imekuwa ikinunua mwani aina ya Ulva kwa Shilingi 800 kwa kilo.

Akijibu swali jingine la mwakilishi huyo, waziri huyo alisema wizara yake inatambua umuhimu wa kuwapo kwa Kamusi ya Viumbe Baharini na kwamba Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar ipo kwenye mchakato wa uchapishaji wake.

Alisema kamusi hiyo itachapishwa kwa lugha nyepesi na inayofahamika na wananchi wengi ambayo ni Kiswahili.

Waziri huyo, alisema kwa sasa taasisi hiyo inatumia kamusi iliyochapishwa kwa lugha ya kigeni yenye viumbe wa bahari wa ukanda wa magharibi ya Bahari ya Hindi.

# Japan yaipiga jeki SMZ

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inathamini michango inayotolewa na wadau wa maendeleo kuwekeza katika miradi ya elimu visiwani hapa

Mahmod aliyasema hayo juzi wakati akizindua ukarabati wa mradi wa jengo la Shule ya Msingi Kizimkazi Wilaya ya Kusini Unguja, anakotoka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema ujenzi huo uliofadhiliwa na Serikali ya Japan unadhihirisha nchi hiyo inaendelea kushirikiana na Zanzibar katika nyanda mbalimbali ili kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema Japan iko mstari wa mbele kuipa misaada ya maendeleo SMZ ikiwamo ya elimu, maji na mingine kutokana na uhusiano wa kindugu.

"Wajapan wengi wanaokuja Zanzibar hujisikia kama wapo nyumbani, hivyo kuna haja kwa wadau hao kuwekeza visiwani katika miradi ya maendeleo," alisema Ayoub.

Alisema Japan ni nchi inayojumuisha visiwa 4,000 na imekuwa na ustaarabu na utamaduni kutoka baharini na inafurahia baraka za bahari kama vile za Zanzibar.

Mkuu huyo alisema uamuzi wa nchi hiyo kutoa msaada wa Sh. milioni 285 kwa ujenzi wa madarasa ya shule hiyo ni wa kishujaa na wa kuigwa.

Alisema moja ya malengo ya SMZ ni kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa madarasa ya kisasa ili kuboresha mazingira ya wanafunzi kusoma na kupunguza msongamano.

Bazozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa, alisema serikali yake ina ushirikiano mzuri wa maendeleo na Tanzani ikiwamo Zanzibar na ndiyo sababu wakaona kuna haja ya kujenga shule hiyo ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri.

Misawa, alisema ujenzi wa shule hiyo ulitiwa saini Machi mwaka jana

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja, Juma Mhammed Chande, alisema mkataba wa ujenzi wa shule hiyo umetokana na fedha kutoka kwa Serikali ya Japan kiasi cha Sh. milioni 285.

Akisoma risala kwa niaba ya walimu wa shule hiyo, Rehema Kassim Ramadhan, alisema kukamilika kwa ujenzi huo kutaondoa changamoto ya ufinyu wa madarasa shuleni hapo na wanafunzi kusoma kwa bidii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**VICTOR EMMANUEL SINDAKILA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1094/0319 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **JIHAD SEKONDARI** mwaka 2008. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/24778/2024.**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED, I , MOHAMEDI SHABANI TINGISHA of DAR ES SALAAM, DO HEREBY** Wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former name of **MOHAMED SHABANI** as it appears in my **PENSIONS FUND (PPF) FOR THE REASON THAT, T**here was typing error occurred during registration of the identity before of writing the full name of **MOHAMEDI SHABANI TINGISHA** the only write two names which are **MOHAMED SHABANI** at that position and from now on I want to use and to be known as **MOHAMEDI SHABANI TINGISHA** and as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of **MOHAMEDI SHABANI TINGISHA** as I appears in my National Identity Card (NIDA).

For the purpose of evidence such determination, I , hereby **DECLARE** that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all public and private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of **MOHAMEDI SHABANI TINGISHA** as my name in lieu of and in substitution of my former name of MOHAMED SHABANI.

**AND I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of **MOHAMEDI SHABANI TINGISHA.**

**IN WITNESS WHEREOF** I have set my hand at Dar es salaam, and I hereon substitute my old name of **MOHAMED SHABANI** by my new name **MOHAMEDI SHABANI TINGISHA.**

SIGNED and DELIVERED by the said **MOHAMEDI SHABANI TINGISHA** who is known to me personally/~~identified~~ to me by ............ the latter being known to me personally in my presence this..11..day of....JAN 2024

DEPONENT



BEFORE ME:
Signature:
Postal address: 45329, DAR-ES-SALAAM
Qualification: ADVOCATE AND COMMISSIONER FOR OATH

EPHRAIM GEORGE NDOSSY ADVOCATE, NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P. O. Box 45329, DAR ES SALAAM

## SHAMBA LINAUZWA LAND FOR SALE

**UKUBWA: 1.6 Acre**
**MAHALI: 400m from Dolly ESTATE**
**Off Moshi-Arusha road 6km from Maji ya Chai**
**AVAILABLE:** Surface water for irrigation 24hrs; Water tank; metallic structure; Access to Electricity; Road access North, south and west

**CONTACT: 0621 30 92 05/0758 88 94 04/0693 72 50 46/ +260 773042039**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATERN YAKOBO LUMBANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 215 AFU** aina ya **RANGE ROVER V8.** Chassis namba **SALLMAMA35A**. Engine namba **512733410.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **KW/RB/673/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHRISTOPHER RWAKILIMBA KAMUGISHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 227 ADF** aina ya **TOYOTA RAV4.** Chassis namba **SXA117011143.** Engine namba **3S7004321.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/27324/2024.**

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai Ndoa Na. 40/2024**
**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK**
**Jina la Mdaiwa: AISHA ABDALLAH**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: AISHA ABDALLAH**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 28 Mwezi wa 03 Mwaka 2024 saa 4:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **27 Mwezi wa 02 Mwaka 2024.**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI WADAIWA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA MJINI**
**WILAYA YA KAHAMA**
**SHAURI LA TALAKA NAMBA 24 YA 2024**

**MDAI HONEST SERAPHINE MREMA**
**AMDAI**
**MDAIWA. JACKLINE DEUS MAJENGE**
**KWA. JACKLINE DEUS MAJENGE**
**MBEZI-DAR ES SALAAM**

**Nyote mlioorodheshwa hapa chini(yaani)**

**JACILLINE DEUS MAJENGE WA MBEZI-DAR ES SALAAM**
Na yeyote atakae liona tangazo hili, awajulishe watu hao waliotajwa hapa juu wahudhurie binafasi katika Mahakama hii ya Mwanzo MJINI siku ya IJUMAA Tarehe 15/3/2024 saa 2:00 Asubuhi, ili mjibu madeni yaliyoletwa na mdaiwa wenu kuwa; **KUJIBU MADAI YA TALAKA.**

Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kuitwa shauri hilo mnatakiwa mje na vielelezo vyenu viwezavyo kuuthibisha utetezi wenu mlionao.
**ANGALIA;** Kama hamkuhudhuria siku na Saa iliotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa Tangazo hili lilibandikwa wazi katika maeneo ya makao yenu na jamaa zenu ambao wanaweza kuwapa taarifa ya kuitwa kwenu, Mahakama itatoa hukumu bila ninyi kuwepo kuwa mmeshindwa. Hati hii imetolewa kwa Amri yangu kwa mujibu wa fungu la 19(2) cha Kanuni za Utaratibu wa madai katika Mahakama za Mwanzo, na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 28/2/2024.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MWANDAMIZI
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KAHAMA MJINI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai Na. 74/2024**
**JINA LA MDAI: RAYMOND ROBERT SAMBAI**
**JINA LA MDAIWA .................... PLATINUM CREDIT LIMITED**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA**
**PLATINUM CREDIT LIMITED**
**MAJENGO – DODOMA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TSH. 12,000,000/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 mwezi 02 mwaka 2024 saa 8:30 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

HAKIMU
PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

**9FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE APPEAL CAUSE NO. 1108 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE EVARESTA MKUNDE**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY REGINALD SIMON MAKOKO**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of 03, 2024.
DATED at DAR ES SALAAM this 22 day of 02, 2024.

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TEREZIA ISAKA KINANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 531 DCM** yenye Chassis namba **MD625AF42MIKO2972** na Engine namba **DF4KM1402558.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/27476/2024.**

Rungwe Avocado Company

## KUPOTEA KWA KADI ZA MATREKTA

**MECK JOHN MWAKIHABA** anatangaza kupotea kwa kadi za matrekta

1. Merssey Ferguson T260PK Chassis No-K25079 Engine No-
2. Merssey Ferguson T417AZD, Chassis No- Engine No-

**TAARIFA YA POLISI NO: PHQ/MBE/RUN/3481/2024**

WAKULIMA TEA COMPANY LIMITED
TUKUYU-RUNGWE
KATUMBA & MWAKALELI

## KUPOTEA KWA KADI ZA MATREKTA

**MECK JOHN MWAKIHABA** anatangaza kupotea kwa kadi za matrekta

1. Merssey Ferguson T440CCB Chassis No-5011P38039 Engine No-U355182T
2. Merssey Ferguson T439CCB Chassis No-5011R19150 Engine No-U397103U

**TAARIFA YA POLISI NO: PHQ/MBE/RUN/3475/2024**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie***
***+255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Tshisekedi akubali kukutana na Kagame

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi, amekubali kukutana na kiongozi wa Rwanda, Rais Paul Kagame, kwa ajili ya mazungumzo ya kutafuta amani vita mashariki mwa nchi hiyo.

Taarifa iliyotolewa katika mtandao wa kijamii wa X, wa ofisi ya rais, ilimnuku waziri wa mambo ya nje wan chi hiyo, Tete Antonio, kuwa Rais Tshisekedi amekubali kukaa meza moja ya mazungumzo na Kagame.

Hata hivyo, Serikali ya Rwanda na Angola hazikutoa taarifa yoyote kuhusu mkutano huo.

Awali nchi mbalimbali zilitoa wito kwa viongozi wa nchi hizo wakutane na kujadili kuhusu utatuzi wa mgogoro huo.

Rais Tshisekedi wakati akifanya kampeni zake mwishoni mwa mwaka jana, alisema hawezi kuzungumza na Kagame, isipokuwa mbele ya Mungu ambaye atatoa hukumu.

Kauli hiyo ilitolewa baada ya juzi kufanyika kwa mkutano uliodumu kwa saa tatu katika mji mkuu wa Angola wa Luanda.

Mkutano huo uliwakutanisha marais wa DRC, Felix Tshisekedi na wa Angola, Joao Lourenco, ambaye ni mpatanishi wa mgogoro huo.

Wakati wa kikao cha Umoja wa Afrika nchini Edhiopia, Rais Lourenco alikutana kwa nyakati tofauti na viongozi hao katika harakati ya kutafuta uwezekano wa kukutana na kufanya mazungumzo ya pamoja.

Katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika mjini Kinshasa wiki iliyopita, Rais Tshisekedi alisema kamwe hatazungumza na waasi wa M23 na badala yake mtu pekee ambaye anataka kuzungumza naye ni Rais Kagame.

Katika ripoti ya wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN) na DRC wanaishitumu Rwanda kwa kusaidia waasi wa M23 wanaopigana mkoa wa Kivu Kaskazini.

Hata hivyo, Rwanda inakana madai hayo.

Upande mwingine Rwanda ina ripoti ya wataalamu wa Umoja wa Mataifa pia inaishutumu DRC kwa kufanya kazi na kundi la waasi wa wanaoendesha harakati zao mashariki mwa Congo (FDLR), ambao Rwanda inadai walihusika na mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 na wanaotaka kuipindua serikali ya Rwanda.

Pia madai hayo DRC imeyakanusha na kusema ya kutungwa.

Wakati huo huo, Umoja wa Mataifa umeanza kuondoa vikosi vya kulinda amani vya nchini DRC (MONUSCO) kwa kukabidhi kituo cha kwanza cha Umoja wa Mataifa kwa jeshi la polisi la nchi hiyo.

Katika sherehe rasmi kuwaaga iliyofanyika katika kambi ya Kamanyola, karibu na mipaka ya Rwanda na Burundi, bendera za Umoja wa Mataifa na Pakistan zilibadilishwa na kupandishwa za DRC.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imetaka kuondolewa kwa wanajeshi hao licha ya wasiwasi wa Umoja wa Mataifa kuhusu ghasia mashariki mwa nchi hiyo kuongezeka.

Nchi ya DRC inalichukulia jeshi la Umoja wa Mataifa kama lisilo na ufanisi katika kuwalinda raia dhidi ya makundi yenye silaha na wanamgambo ambao wanaendelea kupigana mashariki mwa nchi hiyo.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipiga kura mwezi Disemba kuharakisha kuondolewa kwa ujumbe wa MONUSCO, ambao uliwasili nchini humo mwaka 1999.

Umoja wa Mataifa kwa sasa ina wanajeshi 13,500 na polisi 2,000 katika majimbo matatu ya mashariki ya Ituri, Kivu Kusini na Kivu Kaskazini.

Kabla ya mwezi Mei, kikosi cha Umoja wa Mataifa kitaondoka katika kambi zake 14 katika jimbo hilo na kukuabidhi vikosi vya usalama vya DRC. **BBC**




Waandamanaji wakikusanyika karibu na majengo ya Bunge la Nigeria katika mji wa Abuja kupinga kupanda kwa gharama ya maisha nchini humo jana. **PICHA: AFP**

## Amadou Bah ateuliwa waziri mkuu Guinea

**CONAKRY,** GUINEA

SERIKALI ya kijeshi nchini Guinea imemteua Amadou Oury Bah kuwa waziri mkuu mpya baada ya kuvunjwa baraza la mawaziri na kusababisha wafanyakazi kuitisha mgomo.

Katika hotuba kupitia televisheni, kiongozi utawala huo wa kijeshi, Kanali Mamady Doumbouya, alisema Oury Bah, ambaye ni mchumi na aliyekuwa kiongozi wa upinzani, ameteuliwa kushika wadhifa huo kama mkuu wa serikali.

Doumbouya aliongeza kuwa waziri mkuu huyo mpya atapewa jukumu la kushughulikia mvutano na vyama 13 vya wafanyakazi vilivyoitisha mgomo wa nchi nzima ulioanza jumatatu. Vyama vya wafanyakazi vinashinikiza kuachiliwa huru kwa katibu mkuu wa muungano wa wanahabari wa Guinea Sekou Jamal Pendessa, kushuka kwa bei ya vyakula, kuondolewa kwa udhibiti wa vyombo vya habari na mtandao wa intaneti .

Shule, maduka, masoko na barabara katika mji mkuu Conakry zimebaki tupu huku hospitali zikitoa huduma ka dharula pekee. **DW**

## Marekani, Ulaya wakana kupeleka majeshi Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI na washirika wake wakuu wa Ulaya wamesema hawana mpango wa kupeleka wanajeshi nchini Ukraine.

Kauli hiyo imetolewa siku moja baada ya ya Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron kueleza kuwa hajaondoa uwezekano wa kupeleka wanajeshi nchini Ukraine.

Msemaji wa baraza la usalama la kitaifa la Marekani Adrienne Watson, alisema katika taarifa yake kuwa Rais Joe Biden ameshaweka wazi kuwa nchi yake haitotuma wanajeshi kwa ajili ya kupigana nchini humo.

Kauli kama hiyo ilitolewa na nchi za na Ujerumani, Uingereza, Poland na Jamhuri ya Czech ambazo zimejiweka mbali na pendekezo lolote la kuwapeleka wanajeshi nchini Ukraine.

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, alisema hakuna mabadiliko yoyote katika msimamo uliokubaliwa kuwa hakuna nchi yoyote ya Ulaya au nchi mwanachama wa NATO itakayopeleka wanajeshi wake nchini humo.

Waziri wa ulinzi wa Ujerumani Boris Pistorius, alisisitiza kauli hiyo Scholz akisema kupeleka wanajeshi nchini Ukraine sio chaguo la nchi yake.

"Kupeleka wanajeshi nchini Ukraine sio chaguo kwa Ujerumani," Pistorius amewaambia waandishi wa habari wakati wa ziara yake mjini Vienna.

Katibu Mkuu wa muungano wa kujihami wa NATO, Jens Stoltenberg, alikanusha kwamba wanaangalia namna ya kupeleka wanajeshi kwenye uwanja wa mapambano nchini Ukraine.

Hata hivyo, Stoltenberg alieleza kuwa muungano huo wa NATO utaendelea kuiunga mkono Ukraine licha ya nchi hiyo kutokuwa mwanachama.

Awali, Rais wa Ufaransa, Emanuel macron alieleza kuna uwezekano wa mataifa ya Magharibi kupeleka wanajeshi nchini Ukraine siku za usoni japo alisema kutokuwepo kwa makubaliano kuhusu suala hilo.

Ikulu ya Russia imeonya kuwa hatua yoyote ya kujaribu kupeleka wanajeshi wa mataifa ya Magharibi nchini Ukraine itasababisha mzozo huo kutanuka na kuwa kati ya Russia na NATO. **DW**

# JKT YAJUTIA SARE NA KMC

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la klabu ya JKT Tanzania limesikitishwa na sare waliyoipata kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania bara dhidi ya KMC kwenye mchezo uliochezwa juzi uwanja wa Meja Jenerali Isamhuyo, Mbweni, Dar es Salaam.

Katika mchezo huo, JKT Tanzania wakiwa kwenye Uwanja wa nyumbani walilazimishwa sare ya mabao 1-1 na timu hiyo ya manispaa ya Kinondoni.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu JKT Tanzania, Malale Hamsini alisema wachezaji wake walipata nafasi nyingi lakini walishindwa kuzitumia na kusababisha kupata matokeo hayo.

"Sijafurahishwa na matokeo tuliyoyapata, lengo lilikuwa kupata pointi tatu kwenye uwanja wetu wa nyumbani bahatimbaya haijawa hivyo, tulipata nafasi nyingi za wazi tumeshindwa kuzitumia," alisema Hamsini.

Alisema mchezo huo ulikuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa lakini walikuwa na nafasi ya kuondoka na ushindi kama wachezaji wake wangekuwa makini na nafasi walizozipata.

Alisema baada ya mchezo huo kwa sasa anaelekeza nguvu zake kwenye mchezo wao ujao dhidi ya Kagera Sugar watakaocheza Machi 3 kwenye uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Alisema wanajipanga kwa ajili ya mchezo huo wa ugenini na hawatakubali kupoteza tena pointi.

"Malengo yetu ni kupata pointi tatu katika mchezo huo tutapambana kuhakikisha hatupotezi pointi, ninaendelea kuyafanyia kazi makosa niliyoyabaini kwenye mchezo uliopita," alisema Kocha huyo.



Vijana wa Seven Elite Academy (jezi nyekundu), na vijana wa Las Vegas Centre, wakiwania mpira wakati wa michuano ya Busti Kipaji yaliofanyika Uwanja wa Mabibo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kikapu Zanzibar kuandaa kongamano

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

RAIS wa muda wa Shirikisho la mpira wa Kikapu Zanzibar (BFZ) Abdulatif Ali Yasin, amesema wapo kwenye mchakato wa kuandaa kongamano maalum lenye lengo la kurejesha hamasa ya mchezo huo na kutanua wigo wa mchezo huo.

Akizungumza jana na Nipashe, Yasin alisema kongamano hilo litawashirikisha wadau mbalimbali wa mchezo ikiwemo wachezaji wa zamani wa mchezo huo wa Zanzibar.

Alisema lengo kubwa ni kuhakikisha wanachagiza kuinua mchezo huo kuanzia ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa kwa kuwa na mashindano mbalimbali katika ngazi hizo.

Alisema kuwa mchezo huo wa mpira wa kikapu kwa Zanzibar unachezwa na vijana wengi hasa kuanzia umri chini ya miaka 17 hivyo itasaidia kuwapa hamasa ili kucheza mchezo huo kwa malengo badala ya kufanya kama mazoezi.

"Kongamano hili litaenda sambamba na harambee ya kuchangia mchezo huu kutoka kwa wadau watakaokuwepo na wale ambao watapenda kuchangia mawazo yao kwa njia ya maandishi linaendelea kuandiwa kwa kutafuta ufadhili wa wadau mbalimbali," alisema Yasin na kuongeza,

"Tunataka kuunyanyua mchezo huu wa kikapu mpaka kufika ngazi za juu, hili tutafanikiwa iwapo kutakuwa na ushirikiano wa karibu kutoka kwa wadau wa michezo", alisema .

Aidha alisema kuwa katika kipindi hiki cha miaka miwili Shirikisho hilo limedhamilia katika kuhakikisha kuna kuwa na Ligi za Vijana kuanzia umri wa chini ya miaka 17, 20 na 23 kwa jinsia zote.

Aliwaomba wadau wa michezo kushirikiana na Shirikisho hilo katika kuhakikisha wanatimiza malengo yao waliyojipangia katika miaka miwili ambayo wapo madarakani kuliongoza Shirikisho hilo.

## Dar Swiming wajifua mashindano ya Vijana

**Na Shufaa Lyimo**

WAOGELEAJI wa klabu ya Dar Swimming wanaendelea kujifua kujiandaa na mashindano ya vijana ya kuogelea 'Isamilo Invitation Gala' yatakayofanyika kuanzia Machi 8-9 kwenye bwawa la Isamilo mkoani Mwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Klabu hiyo, Radhia Shabani alisema mashindano hayo yatashirikisha vijana wenye umri tofauti tofauti kutoka katika klabu za mikoa mbali mbali ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema lengo la mashindano hayo ni kuangalia uwezo wa waogeleaji katika kutumia bwawa la mita 50.

"Kwa upande wetu tumejipanga vizuri kuhakikisha tuna kwenda kushindana na si kushiriki, vile vile tutaweza kupata waogeleaji wenye uwezo wa kumaliza bwawa la mita 50 pamoja na kupunguza muda wao katika uogeleaji," alisema Shabani.

Aidha, alisema hana wasi wasi na waogeleaji wake kwani anawapa mazoezi ambayo yatawafanya wakaitangaze vema klabu yao hiyo.

Alisema waogeleaji wote wana morali ya juu kwani kila mmoja anayatamani mashindano hayo ambayo yanatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa.

Wakati huo huo Meneja wa klabu hiyo, Inviolata Itatiro aliwataka wazazi wawaruhusu watoto wao wajifunze mchezo huo kwani michezo ni afya vile vile itawasaidia kupata fursa ya kujitangaza nje na ndani ya nchi.

"Wazazi wanapaswa kufahamu huu ni mchezo mzuri, wawalete watoto kwenye Klabu yetu tuna makocha wenye viwango vya hali ya juu ambavyo vimeweza kuwainua waogeleaji wengi hapa nchini," alisema Itatiro.

# *Shime alia na uzoefu Twiga Stars*

**Na Saada Akida**

KOCHa wa Timu ya Taifa ya Wanawake 'Twiga Stars', Bakari Shime, amesema ukosefu wa uzoefu ni sababu kubwa ya kuondolewa na Afrika Kusini 'Banyanabanyana' kwenye michuano ya kufuzu michezo ya Olimpiki.

Twiga Stars imetupwa nje ya michuano hiyo kwa jumla ya mabao 4-0, baada ya juzi kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini ikiwa siku chache tangu wakubali kipigo cha nyumbani cha mabao 3-0 na wasauzi hao.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema kwa ujumla wamecheza vizuri kwenye mchezo wa juzi tofauti na mchezo wa kwanza kwa kuonyesha upambanaji wa juu na kutengeneza nafasi nyingi lakini walishindwa kuzitumia kutokana na umakini mdogo uliochangiwa na kutokuwa na uzoefu kwa baadhi ya wachezaji wake.

Alisema anaimani wametolewa katika mashindano hayo lakini wamefaidia na kupata mechi nzuri ambazo inaweza kuwa chagizo kwao kwa ajili ya michuano iliyopo mbele yao ikiwa pamoja na fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON) ambayo Twiga Stars wamefuzu kushiriki. "Mategemeo yangu mechi inayofuata tutakuwa bora zaidi ya mechi hii, tunarudi nyumbani kukaa chini kuangalia mapungufu yetu yalikuwa nini kwenye michezo hii miwili na kuyarekebisha.

"Tunatambua tumecheza na timu kubwa, tumejifunza na kutumia mechi hizo mbili kusahihisha makosa yetu na kufanya maandalizi ya kujiandaa na WAFCON," alisema Shime.

Aliongeza kwa sasa wanarejea nyumbani kufanya maandalizi kwa timu ya Wasichana ya U- 20 'Tanzanite' kuelekea michuano ya All Afrika Games ambapo kuna baadhi ya wachezaji wapo katika kikosi cha Twiga Stars na wamepata uzoefu kwenye michezo miwili dhidi ya Afrika Kusini.

Nyota awaliopo kwenye kikosi cha Twiga Stars na pia wameitwa Tanzanite ni kipa Husna Mtunda, Washambuliaji wawili Winifrida Gerald na Christer Bahera (wote kutoka Yanga Princess), Jamila Rajabu , Joyce Lema (JKT Queens), Violeth Nicholaus na Asha Mnuka (Simba), Hasnat Ubamba (Fountain Gate Princess)

Wachezaji wengine ambao hawako Twiga Stars na wameitwa kwenye kikosi cha Tanzanite kwa ajili ya 'All Afrika Games' ni Zulfa Makauo, Lydia Maximilian, Jackline Shija na Alia Fikiri (JKT Queens), Mariam Shaban, Ester Maseke na Jamila Selestine (Bunda Queens).

Wengine ni Sarah Joel (Fountain Gate Princess), Koku Kipanga na Zainabu Mohammed (Simba Queens), Sabina Alex (Geita Gold Queens ), Neema Paul na Asha Omari (Yanga Princess).

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ROBERTSON KUMRITHI DAVIES

MLINZI wa Liverpool na Scotland, Andy Robertson mwenye umri wa miaka 29, ndiye mlengwa mkuu wa mabingwa wa Ujerumani Bayern Munich wakati wakipanga jinsi ya kujaza nafasi ya mchezaji wa kimataifa wa Canada, Alphonso Davies, ambaye anaonekana yuko tayari kujiunga na Real Madrid. (***Daily Mail***)

### JESUS NDIO SABABU

WASIWASI wa Arsenal juu ya kiwango cha majeruhi ya mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus ni sababu kubwa ya kutafuta mshambuliaji mpya, huku Ivan Toney wa Brentford, Victor Osimhen wa Napoli, Joshua Zirkzee wa Bologna na Viktor Gyokeres wa Sporting wakiwa miongoni mwa wachezaji wanaolengwa. (***Daily Mail***)

### HATO ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL wanamtaka beki wa Ajax, Jorrel Hato mwenye umri wa miaka 17, lakini klabu hiyo ya Uholanzi ina matumaini ya kumshawishi asaini mkataba mpya. (***Evening Standard***)

### MDOGO WA MBAPPE NAE ASAJILIWA

KAMA sehemu ya makubaliano ya kumsajili Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25, Real Madrid pia wamekubali kumsajili mdogo wa mshambuliaji huyo wa Ufaransa, Ethan mwenye umri wa miaka 17 kutoka Paris St-Germain. (***OK Diario***)

### ZIDANE KUMRITHI HAG

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane mwenye umri wa miaka 51, yuko juu ya orodha ya Sir Jim Ratcliffe kuchukua nafasi ya Erik ten Hag kama kocha mpya wa Manchester United. (***FootMercato***)

### ZERBI ATAJWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inavutiwa na kocha wa Brighton, Roberto de Zebri, huku Xabi Alonso wa Bayer Leverkusen na kocha wa zamani wa Ujerumani, Hansi Flick pia wanatajwa. (***Sky Germany)***

### KOMPANY HAFUKUZWI

KAZI ya Vincent Kompany haipo mashakani pale Burnley, licha ya timu yake kutarajia kurejea kwenye ligi ya Championships. (***The Athletic***)

### DE GEA AFIKIRIWA BARCA

BARCELONA inafikiria kumnunua mlinda mlango wa zamani wa Manchester United, David de Gea mwenye umri wa miaka 33, huku Mhispania huyo akiwa mchezaji huru kwa sasa. (***Mundo Deportivo)***

### MARMOUSH ANYATIWA

NEWCASTLE United na Tottenham Hotspur zinamtaka mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt mwenye umri wa miaka 25, Omar Marmoush, mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri amefunga mabao 10 katika michezo 18 ya Bundesliga msimu huu. (***Bild via Shields Gazette***)

### VARELA AWANIWA

LIVERPOOL inapania kumsajili kiungo wa kati wa FC Porto na Argentina, Alan Varela mwenye umri wa miaka 22. (***Mirror***)

### INZAGHI ATAJWA BARCA

BARCELONA inafikiria kumchukua kocha wa Inter Milan, Simeone Inzaghi ili kuchukua nafasi ya Xavi, ambaye ataondoka mwishoni mwa msimu huu. (***Mundo Deportivo***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ERLING HAALAND AWAONYA WAPINZANI WA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

**●●● Mshambuliaji huyo juzi alifunga mabao matano peke yake na kusema amerejea kwenye...**

ERLING Haaland ni kama alituma onyo kwa wapinzani wa Manchester City baada ya kufunga mabao matano kwenye ushindi wa 6-2 wa Kombe la FA dhidi ya Luton Town Jumanne, akisema amerejea kwenye ubora wake na kusema "tuko tayari kushambulia."

**Haaland alikuwa amefunga mabao matatu pekee katika mechi saba tangu arejee kutoka kwenye majeraha ya mguu ambayo lilimfanya kuwa nje kwa zaidi ya mwezi mmoja kati ya Desemba na Januari.**

Lakini mshambuliaji huyo wa Norway alirejea katika kilele chake pale kwenye dimba la Kenilworth Road kwa kufunga 'hat trick' kipindi cha kwanza na mabao mawili zaidi baada ya kipindi cha mapumziko City wakitinga robo fainali ya Kombe la FA.

Kwa kufanya hivyo, Haaland alikua mchezaji wa kwanza wa ligi kuu England kufunga mabao matano kwenye mechi ya Kombe la FA tangu George Best alipofunga sita kwa Manchester United dhidi ya Northampton Town mwaka 1970.

"Ninarejea kwenye ubora wangu," aliiambia ITV. "Mwishowe ninajisikia vizuri. Ni hisia ya kushangaza. Inakuja, tunakuja. Nyakati za kusisimua mbele. Tuko tayari kushambulia."

Ilikuwa ni mara ya pili kwa Haaland kufunga mabao matano katika mchezo mmoja ndani ya msimu mmoja na nusu pekee akiwa na City baada ya kufanya hivyo hivyo katika ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 sasa ana mabao 79 katika mechi 83 alizochezea Man City katika mashindano yote.

Mabao manne ya kwanza ya Haaland dhidi ya Luton yalikuja kwa msaada kutoka kwa Kevin De Bruyne, ambaye pia amekosa sehemu kubwa ya msimu huu kutokana na kuwa majeruhi.

"Ni furaha kucheza naye," aliongeza Haaland. "Nadhani tunajua sisi sote tunataka nini kutoka kwa kila mmoja, tunatazamana na inabofya vizuri."

Uchezaji wa Haaland na uchezaji wa kiungo De Bruyne pia utachochea imani kuwa City inaweza kurudi kubeba mataji matatu ya msimu uliopita waliposhinda taji la Ligi Kuu, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Erling alikuwa moto na Kevin alikuwa kamili," alisema Kocha wa Man City, Pep Guardiola.

"Muunganisho walio nao. Erling anahitaji mchezaji kama Kevin na Kevin anahitaji mchezaji kama Erling."

Mateo Kovacic pia alifunga bao kwa Mabingwa City, ambao hawajafungwa katika mechi 18 katika mashindano yote.

Mechi ya mkondo wa pili itafanyika Machi 6, baada ya City kucheza na wapinzani wao wa jiji moja, Manchester United kwenye Ligi Kuu Jumapili.



# TEN HAG: SIJALI KAMA NITATIMULIWA

**MANCHESTER,** England

KOCHA Erik ten Hag amesema hajali kwamba mmiliki mpya Sir Jim Ratcliffe bado hajathibitisha hadharani kuwa atabakia kama kocha wa Manchester United msimu ujao.

Kocha huyo wa United ana mkataba Old Trafford hadi mwaka 2025 lakini kumekuwa na uvumi kuhusu nafasi yake baada ya msimu mbaya ambapo timu yake imeporomoka hadi nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Asilimia 27.7 ya hisa za Ratcliffe katika klabu hiyo zilithibitishwa wiki iliyopita, lakini bilionea huyo wa England mwenye umri wa miaka 71, amekataa kuthibitisha kama Ten Hag atakuwa kocha msimu ujao.

Hata hivyo, Mholanzi huyo amesisitiza kuwa sio tatizo na amesema timu mpya ya usimamizi "anaamini" yeye ndiye mtu sahihi kwa kazi hiyo.

Alipoulizwa kama itakuwa na manufaa kwa Ratcliffe kuthibitisha kuwa atabakia kama kocha, Ten Hag alisema: "Niko chini ya mkataba wa misimu mitatu, hivyo sijali.

"Niko kwenye mchakato huu, nazingatia mchakato tu, kwa hiyo sijali kinachoendelea karibu yangu. Nina mazungumzo mengi na Sir Jim Radcliffe, pia na Sir Dave Brailsford na wengine katika kundi hilo, kwa hivyo wanajua tunapozungumza na nina imani kubwa na ninahisi kwamba wananiamini."

Ratcliffe anapanga mabadiliko kadhaa ndani ya United na tayari amemchukua Omar Berrada kutoka Manchester City kama Mkurugenzi Mtendaji mpya wa klabu hiyo. Pia amemtafuta Mkurugenzi wa Michezo wa Newcastle United, Dan Ashworth na bado kuna nia ya kumtaka Jason Wilcox wa Southampton ajiunge na timu ya kuajiri.

Hatua hizo zimesababisha mapendekezo kwamba Ratcliffe na timu yake wanafuatilia kwa ufupi kuhusu Ten Hag, lakini kocha huyo mwenye umri wa miaka 54 alisema hajisikii kuwa yuko kwenye majaribio.

"Hapana, lakini nataka kushinda kila mchezo," alisema. "Najua niko kwenye mchakato, najua ninachofanya. Kama nilivyosema tu, nimekuwa na mazungumzo mengi, mara kwa mara tuna mazungumzo, na tunazungumza juu ya siku zijazo pamoja.

"Ninazingatia pointi hizo mbili, kuendeleza timu katika wakati huu na mchezo unaofuata, na kufikiria juu ya siku zijazo na kufanya hivyo kwa pamoja."

Kipigo cha 2-1 kutoka kwa Fulham Jumamosi kiliiacha United kwa pointi nane kutoka kwenye nafasi nne za juu nafasi ambazo zinakuhakikishia kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.



## Aguero akanusha kurudi kucheza

**BUENOS AIRES,** Argentina

SERGIO Agüero amekanusha ripoti kwamba, atafanya mazoezi na klabu ya Independiente ya Argentina ili kurudi tena kucheza baada ya kustaafu soka.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Argentina alistaafu soka Desemba 2021 alipokuwa Barcelona akiwa na umri wa miaka 33 kutokana na ugonjwa wa moyo.

"Ni uongo kabisa, sitafanya mazoezi na Independiente," alisema Agüero.

"Wakati mwingine mambo yanavumishwa tu. Sijui kwa faida ya nani. Narudia tena kuwa daktari wa magonjwa ya moyo alisema niko mzima, ni muhimu kuwa na afya njema. Lakini ili nirudi kwenye mazoezi ya kucheza mpira, nitahitaji kufanyiwa vipimo vingi."

Mfungaji huyo bora wa muda wote wa Manchester City, Agüero alianza maisha yake ya soka la ujana akiwa na Independiente.

Hivi majuzi Agüero alinukuliwa kwenye Twitch atalazimika "kushauriana na daktari wake wa moyo" ikiwa kocha wa Independiente, Carlos Tevez atampigia simu.

Tevez alijibu kwamba timu yake ingemkaribisha Agüero kwa mikono miwili.

"Nani hataki kuwa na Kun? Kwanza mimi kama mchezaji mwenzake, na sasa kama kocha," aliema Tevez kuhusu mchezaji mwenzake wa zamani wa Man City na Argentina.

# Chelsea wapata pigo lingine kwa Nkunku

**LONDON,** England

CHELSEA imepata pigo jipya la jeraha kwa Christopher Nkunku ambaye atalazimika kuwa nje ya dimba kwa wiki kadhaa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 ameichezea The Blues mara tisa pekee msimu mzima, kutokana na jeraha baya la goti alilolipata Agosti na tatizo la nyonga alilopata Januari.

Nkunku aliingia akitokea benchi wakati wa mechi ya fainali ya Kombe la Carabao Jumapili dhidi ya Liverpool kwenye Uwanja wa Wembley, lakini hakuweza kucheza huku vijana wa Mauricio Pochettino wakipoteza mchezo kutokana na bao la dakika za mwisho la Virgil van Dijk. Katika pigo zaidi kwa Pochettino, kocha huyo wa zamani wa PSG na Tottenham Hotspur atakosa tena huduma ya Nkunku, akifichua katika mkutano wake na waandishi wa habari kuwa jeraha limemtokea tena.

"Tunahitaji kuona na kutathmini kila siku, lakini atakuwa nje kwa wiki tatu au nne," alisema kocha huyo raia wa Argentina. "Tunatumaini hakuna zaidi.

"Ni ngumu kwake. Tulimtazama alipofika kwenye mazoezi. Alikuwa akiruka kwenye uwanja wa mazoezi hadi akajeruhiwa. Sasa ni karibu miezi nane na amehusika tena lakini si mchezaji yule yule wa awali."

Nkunku alikuwa mmoja wa wachezaji waliosajiliwa na Chelsea majira ya joto, na kuigharimu klabu hiyo pauni milioni 52, lakini hajaweza kuonesha kiwango chake pale Stamford Bridge.

Mfaransa huyo amefunga mara mbili pekee katika mechi tisa, huku mapambano yake ya utimamu yanaendelea kuathiri uwezo wake wa kuendelea kuoyesha kipaji chake uwanjani.



## Kocha Mtibwa alia utulivu kwa washambuliaji wake

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema kazi aliyonayo kwa sasa ni kuwatengeneza kisaikolojia washambuliaji wake ili wawe watulivu wanapokuwa langoni kwani wanapoteza nafasi nyingi za kufunga.

Akizungumza juzi, baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Manungo Complex, Turiani, Morogoro dhidi ya Dodoma Jiji ambayo walitoka suluhu, Katwila alisema timu yake ingeweza kuibuka na ushindi katika mchezo huo, lakini washambuliaji wake walikuwa wakibabaika na kushindwa kuwa na utulivu kila walipokuwa kwenye nafasi ya kuuweka mpira wavuni.

"Najua hii yote ni kwa sababu hatushindi mechi zetu, tunapitia kwenye wakati mgumu kiasi kwamba wachezaji wanapokuwa kwenye nafasi ya kufunga wanatetemeka na kupoteza nafasi, hili ni suala siyo tena la kiufundi ila ni la kisaikolojia, itabidi nikae nao nione jinsi gani ya kuwasaidia, huku kwenye ufundi tumejitahidi sana, timu inacheza vizuri,wachezaji wangu walipambana, walitumia ufundi, nguvu, na kila kitu, lakini wenzetu wameweza kutuzuia vizuri, ndiyo mpira, hatupo kwenye wakati mzuri, inabidi kuendelee kupambana," alisema Katwila.

John Baraza, Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji kwa upande wake alishangaa kwa jinsi Mtibwa walivyocheza katika mechi hiyo tofauti na jinsi alivyoizoea na kuisoma.

"Tulijua watakuja kucheza kama tulivyodhani, haikuwa hivyo, walitushambulia kwa nguvu kiasi kwamba ikabidi niweke mabeki watano nyuma badala ya wanne, nawapongeza vijana wangu, pointi moja mimi kwangu ugenini siyo mbaya," alisema Baraza.

Matokeo ya mechi hiyo, yanaifanya Mtibwa kuendelea kuburuza mkia ikiwa na pointi tisa, Dodoma Jiji ikishika nafasi ya 10, ikiwa na pointi 20.



# MSHAMBULIAJI SIMBA AANZA KUTUPIA KMC

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Shaaban Chilunda ambaye yupo kwenye klabu ya KMC kwa mkopo, juzi alifunga bao lake la kwanza katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, akiiokoa timu yake isipate kipigo kutoka kwa JKT Tanzania.

Chilunda aliyesajiliwa na Simba msimu huu na kupelekwa KMC katika uhamisho wa dirisha dogo, alipachika bao dakika ya 40 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya JKT Tanzania mchezo uliochezwa Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1.

Chilunda aliunganisha mpira wa krosi kutoka winga ya kushoto aliunganisha kwa mguu wake wa kushoto mpira ulioenda moja kwa moja nyavuni.

Awali, JKT Tanzania ilitangulia kwa bao lililowekwa wavuni na Najim Magulu dakika ya nane ya mchezo.

Mpaka anaondoka Simba, Chilunda hakufunga bao lolote na sasa bao hilo akiwa na KMC ni bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Kocha Msaidizi wa KMC, John Matambala ameonekana kuridhishwa na sare, akisema mpango wao ulikuwa ni kukaa nyuma na kushambulia kwa kustukiza.

"Kiukweli sare hii si kitu chepesi, ni ngumu kupata hata sare kwenye mechi za sasa za ligi hasa ukicheza ugenini kwa sababu timu imejizatiti kutumia vyema uwanja wake wa nyumbani, tuliingia na mkakati wa kuwaacha wacheze, halafu sisi tutumie mianya watakaoiacha, mpango umefanikiwa ingawa si sana," alisema kocha huyo.

Aidha, Kocha Msaidizi wa JKT Tanzania, George Mketo, alisema waliingia wakijua kuwa KMC ni timu yenye tabia ya kumiliki mpira kutoka chini kwa hiyo waliamini wakiiminya mianya yao, wakiwanyang'anya mpira na kushambulia wanaweza kupata mabao.

"Tulifanikiwa kipindi cha kwanza, lakini na wao kipindi cha pili wakashtuka na kubadilisha mfumo, pamoja na hayo sisi ndiyo tumepata nafasi nyingi na hatukuzitumia," alisema Mketo.

Matokeo hayo yanaifanya KMC kushika nafasi ya tano katika msimamo ikiwa na pointi 24, huku JKT Tanzania ikiwa nafasi ya 12 na pointi zake 18.




Wafanyakazi wa mgodi wa Barrick uliopo mkoani Mara wakishiriki katika mashindano ya mbio za Kilimanjaro International Marathon yaliyofanyika mkoani Kilimanjaro hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wachezaji Yanga waapa kuishangaza Al Ahly kwao

INATOKA UK 24

kuna wachezaji wazuri na kwa sababu mpira ni biashara, basi pamoja na kuipambania timu, lakini watataka kujiuza.

"Tutacheza kama timu na tumeambizana tupambane tupate nafasi ya kwanza, litakuwa jambo zuri kwa upande wetu na wa klabu, hatupo Misri kutembea au kushangaa mataa, tunajua Al Ahly ni timu ngumu, hata mechi zingine tulizocheza nazo zilikuwa ngumu, lakini zilionekana ni rahisi kutokana na umoja wetu na kujituma," alisema Bacca.

## Simba wajipanga hujuma kwa Mkapa

INATOKA UK 24

hofu mashabiki wa timu hiyo kuelekea kwenye mchezo wa Jumamosi kwa kusema maandalizi yamefanyika kikamilifu kuanzia ndani na nje ya uwanja.


"Kwenda robo fainali kunategemea wanasimba wenyewe, tujitokeze kwa wingi uwanjani kuwashangiliia na kuwasapoti wachezaji wetu, Jwaneng ajione mnyonge na yatima," alisema.

Simba inahitaji ushindi wa aina yoyote kujihakikishia kutinga hatua ya robo fainali kwa mara ya tano ndani ya misimu sita ya michuano hiyo ya CAF.

# Michezo

Nipashe

Alhamisi Februari 29, 2024

Erling Haaland awaonya wapinzani UK. 21





Kiungo wa Yanga, Pacome Zouzoua, akimtoka beki wa CR Belouizdad kwenye moja ya mchezo wa Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika, kiungo huyo amepania kuisaidia timu yake kushinda mchezo wao wa mwisho kesho dhidi ya Al Ahly. **PICHA: MAKTABA**

# WACHEZAJI YANGA WAAPA KUISHANGAZA AL AHLY KWAO

## ●●● Pacome asema wanaitaka nafasi ya kwanza kwenye kundi, hivyo...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WACHEZAJI wa Yanga wameapa kuishangaza Al Ahly nyumbani kwa kupambana kuibuka na ushindi kwenye mchezo wao wa mwisho hatua ya makundi (Kundi A) utakaochezwa kesho jijini Cairo, Misri.

Yanga iliondoka nchini juzi kuwafuata vigogo hao wa soka la Afrika lakini wachezaji wamepania kuipambania timu huku kiungo 'fundi' Pacome Zouzoua akiweka wazi kuwa wanaitaka nafasi ya kuongoza kundi hilo.

Ikumbukwe Yanga tayari imefuzu hatua ya robo fainali baada ya ushindi mnono wa nyumbani wa mabao 4-0 dhidi ya CR Belouizdad na sasa ni vita kati yao ya Al Ahly ya kuongoza kundi hili kwani waarabu hao nao wameshafuzu kwa hatua hiyo.

**Kuelekea mchezo huo wa kesho, Pacome, amesema watapamba na ugenini kuhakikisha wanapata ushindi am bao utawafanya waon goze kundi hilo.**

"Tunatambua itakuwa mechi ngumu kwa sababu Al Ahly wapo nyumbani, lakini tumejiandaa vizuri na tunaitaka hii mechi kutafuta ushindi ambao utatufikisha kwenye nafasi ya kwanza kwenye msimamo wa kundi letu, ni jambo tunaloliwaza sasa hivi baada ya kupata uhakika wa kufuzu," alisema Pacome.

Alisema wamejipanga vizuri na wanaendelea kujiandaa na mchezo huo ambao utakuwa wa kuvutia kutokana na aina ya uchezaji wa timu hiyo.

Kauri hiyo iliungwa mkono na beki wa kati wa timu hiyo, Dickson Job ambaye alisema katika kikao kifupi cha wachezaji wameazimia kuweka rekodi nyingine ya kuliongoza Kundi D na hiyo itawezekana kama mikakati waliyopangiana itatekelezwa kikamilifu.

"Sisi kama wachezaji tunaitaka mechi, tumejipanga vizuri, tunahitaji kuwa wa kwanza kwenye kundi kama ambavyo wao wanaitaka, hatuhofii kuwa tunacheza kwao, tumeshavuka kwa hiyo tutacheza soka bila presha, hii itakuwa na faida kubwa kwetu kwani wao wenzetu watataka ushindi kwa lazima ili wawafurahishe mashabiki wao.

"Tumekaa na wachezaji wenzetu, kitu ambacho tumeambiana na inawezekana kuongoza kundi, cha kufanya ni kutofanya makosa hasa kwa sisi mabeki, na kule mbele kila nafasi inayopatikana tuitumie vizuri, hili litatufanya kutimiza malengo ya muda mfupi tuliojiwekea wachezaji ya kuwa vinara wa kundi D," alisema Job.

Aidha, beki mwingine wa kati Ibrahim Hamadi 'Bacca', alisema katika mechi ya kesho wanataka kuonyesha kuwa hata Afrika Mashariki

INAENDELEA UK 23

## Simba wajipanga hujuma kwa Mkapa

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema umejipanga kukabiliana na hujuma ya aina yoyote kutoka ndani au nje ya nchi kwenye mchezo wao wa Jumamosi wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Simba itaumana na Wabotswana hao kwenye mchezo muhimu utakaowahakikishia kufuzu hatua ya robo fainali kama wataibuka na ushindi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, ametoa tahadhari kwa yoyote ambaye atatia mkono kutaka kuihujumu na kuiangusha timu hiyo ili isiende hatua ya robo fainali.

"Tunajua kwenye msafara wa kenge na mamba wapo, tumejipanga kukabiliana na hujuma yoyote na nisema mtu au kikundi chochote kitakachohujumu mchezo huu tutapambana nao," alisema Ahmed.

Ahmed ameitoa kauli hiyo jana kwenye uzinduzi wa hamasa kuelekea katika mchezo huo wa Jumamosi utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Yeyote atakayechezea mechi zetu na kutuhujuma hatakuja kusahau kile tutakachomfanyia, hatosahau yeye wala kizazi chake, tunautaka huu mchezo, tunataka kutinga robo fainali kama ilivyokawaida yetu," alisema Ahmed.

Alisema wanakusanya nguvu zao na kuwa kitu kimoja, kusimama imara kuelekea kwenye mchezo huo wa Jumamosi utakaochezwa saa 1:00 jioni.

"Mpira ni burudani lakini ni vita, unapoingia katika matokeo basi tunaingia katika vita na hatutacheka na mtu, yeyote anayejifanya kiherehere kucheza mechi yetu tutaruka naye vibaya.

"Hii wiki tupo kwenye vita, kila mwana Simba awe mkali, tuhakikishe kazi inabaki uwanjani tu kwa wachezaji wake kutupeleka robo fainali," alisema Ahmed.

Aidha, Ahmed amewatoa

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002